Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo

UMG Kasi na Ubora

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00076 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Julai 31 - Agosti 6, 2024 |

## JKCI Dar Group yazindua mtambo kuzalisha oksijeni



Na Mwandishi Wetu

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)–Hospitali ya Dar Group, imezindua mtambo wa kisasa wa kuzalisha hewa ya oksijeni wenye thamani ya zaidi ya Sh milioni 500. Uk. 2.

## Kituo kurejeleza taka plastiki kujengwa Dom



Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imepanga kujenga kituo cha kurejeleza taka za plastiki pamoja na kuhifadhi na kuchambua taka ngumu kwa ajili ya kutumika kama malighafi ya viwanda. Uk. 2.

## DC Okash na migogoro ya ardhi Bagamoyo



Na Mwandishi Wetu, Bagamoyo

MJI wa Bagamoyo mkoani Pwani ilikuwa bandari muhimu ya biashara ya kimataifa katika karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20.

Mji huu pia ulikuwa kituo cha biashara ya utumwa, jambo ambalo limeacha alama ya kudumu kwenye historia na utamaduni wa eneo hilo. Hadi leo Bagamoyo ni moja ya vivutio vya utalii, ukijulikana kwa majengo ya kale, maeneo ya kihistoria na utamaduni... Uk. 3.

MAKALA

**Hatari za kiafya za kuweka kope bandia** Uk. 7



**Wagombea uongozi TLS waahidi makubwa** Uk. 10



**Vigingi vinavyomsubiri Tundu Lissu nia yake ya urais** Uk. 12



### BIMA YA AFYA KWA WOTE:

# Uswisi yamuunga mkono Dk. Samia

Uk. 4



## ... Kesho kuzindua safari SGR D'Salaam Dodoma

Uk. 4



**Kimataifa** RSF wameua watu 65 katika mji wa El-Fasher | Kamanda wa mamluki la Urusi auawa Uk.19

# Samia ziarani mkoani Morogoro siku tano

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, anatarajia kuanza ziara ya kikazi ya siku tano mkoani Morogoro kuanzia Agosti 2, mwaka huu.

Akiwa mkoani humo, Rais Dk. Samia mbali na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo, pia atazungumza na wananchi.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

# JKCI Dar Group yazindua mtambo kuzalisha oksijeni




**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)–Hospitali ya Dar Group, imezindua mtambo wa kisasa wa kuzalisha hewa ya oksijeni wenye thamani ya zaidi ya Sh milioni 500.

Mtambo huo ulionunuliwa nchini Uturuki, utapunguza gharama za ununuzi wa oksijeni kutoka katika vituo vingine.

Ulikabidhiwa kwa JKCI-Dar Group na Umoja wa Mabenki Tanzania (TBA) ambapo kiasi cha Sh. milioni 320 zilitumika kuunua na Sh. milioni 70 kwa ajili ya kasha la kuhifadhia mtambo, usafirishaji na Sh. milioni 136 kwa ajili ya kusimika na kusambaza hewa wodini na sehemu nyingine zenye uhitaji.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji JKCI Dk. Delila Kimambo, alisema mtambo huo unatumia umeme na kuzalisha hewa ya oksijeni yenye ujazo wa milimita za mraba 21 yenye kasi ya mita tano kwa saa wakati wa kujaza.

"Una vifaa vingi ndani yake vikiwemo kifaa cha kupima ubora wa oksijeni, kifaa cha kujaza hewa, tangi la kupokea hewa la lita 1,000," alifafanua.

# Kituo kurejeleza taka plastiki kujengwa Dom

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepanga kujenga kituo cha kurejeleza taka za plastiki pamoja na kuhifadhi na kuchambua taka ngumu kwa ajili ya kutumika kama malighafi ya viwanda.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye kipindi cha 'Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo' kinachotayarishwa na ofisi yake kurushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Alisema kituo hicho kitakachojengwa jijini Dodoma, kitasaidia ukusanyaji wa taka kutoka dampo kwa ajili ya kuchakatwa hatua itakayosaidia kulinda mazingira.

Alisema kuwa si kazi za viwandani pekee ndizo zinazozalisha gesijoto angani, lakini pia shughuli mbalimbali za kila siku za mwanadamu ni chanzo cha uzalishaji wa gesijoto hiyo.

"Shughuli zetu za kila siku za nyumbani, ofisi tunatupa taka tunazikusanya na zikichukuliwa kupelekwa dampo zinazalisha gesijoto ambayo ina athari kubwa katika mazingira yetu na hatimaye kutuletea changamoto ya mabadiliko ya tabianchi," alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji

# DC Okash anavyopambana kumaliza migogoro ya ardhi Bagamoyo

**Na Mwandishi Wetu, Bagamoyo**



**Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, akiwa kwenye moja ya mikutano ya Operesheni Mapinga Ondoa Migogoro ya Ardhi.**

MJI wa Bagamoyo mkoani Pwani ilikuwa bandari muhimu ya biashara ya kimataifa katika karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20.

Mji huu pia ulikuwa kituo cha biashara ya utumwa, jambo ambalo limeacha alama ya kudumu kwenye historia na utamaduni wa eneo hilo. Hadi leo Bagamoyo ni moja ya vivutio vya utalii, ukijulikana kwa majengo ya kale, maeneo ya kihistoria na utamaduni, mbali na fukwe zake nzuri.

Mengi yamefanyika katika wilaya hii kongwe nchini yakilenga wananchi wake waendelee kukua kimaendeleo na kiuchumi. Kutokana na kupakana na bahari, kuna idadi kubwa ya wananchi wa Bagamoyo ambao wamejikita katika shughuli za biashara za rasilimali za bahari (uchumi wa buluu) lakini pia kuna wakulima na wafugaji.

Wilaya ya Bagamoyo hivi karibuni imekuwa ikitajwa si kwa utalii sana isipokuwa kwa migogoro ya ardhi hususani katika kata ya Mapinga, jambo ambalo limechangiwa na baadhi ya matapeli kuwauzia wahitaji wa ardhi maeneo ambayo tayari yana hatimiliki.

Katika eneo hilo wananchi walio wengi ambao wanatoka mkoa jirani wa Dar es Salam na maeneo mengine ya nchi wamekuwa wakilalamikia kuuziwa maeneo yenye hati miliki na baadhi yao kupata hasara ya kuvunjiwa nyumba zao kutokana na kujenga kwenye maeneo yanayomilikiwa kihalali na watu wengine.

Hali hiyo ilisababisha mawaziri tofauti kutoka Wizara ya Ardhi kufanya ziara Bagamoyo, hususani katika Kata ya Mapinga kusikiliza malalamiko ya wananchi ili kutatua migogoro ya ardhi.

Pamoja na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani kuwa na migogoro ya ardhi katika Wilaya za Kibaha, Kisarawe Mkuranga na Rufiji lakini Bagamoyo imekuwa ikitajwa kuongoza hususani eneo hilo la Mapinga na Makurunge, jambo ambalo ofisi ya Kamishna katika kesi za ardhi za mkoa huo zinazosikilizwa idadi kubwa inatoka maeneo hayo.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash ameanzisha kliniki ya ardhi ambayo ilianza kufanyika katika Halmashauri za Chalinze na Bagamoyo kwa kusikiliza wananchi wenye migogoro akiwa na timu ya watendaji wa ardhi.

Hata hivyo, pamoja na kliniki hiyo Okash aliona bado ipo sababu ya kuanzisha oparesheni maalumu kwenye maeneo yenye migogoro mingi ya ardhi akiwa na timu ya watendaji wa idara ya ardhi, mwanasheria pamoja na watendaji kutoka ofisi ya ardhi ya kila halmashauri.

Jambo analolifanya Okash ni jipya kwa wakazi wa wilaya hiyo na linawezesha wananchi wengi wenye migogoro kujitokeza kupatiwa ufumbuzi kutoka kwa watalaamu wa ardhi na wanasheria kuhusiana na maeneo wanayomiliki.

Pamoja na kufanya kliniki hizo kwenye kila halmashauri mbili za Wilaya ya Bagamoyo, bado Okash anaona kuna malengo hajayafikiwa katika kutatua migogoro kwenye eneo lake na sasa analazimika kuanziasha Operesheni Mapinga Tokomeza Migogoro ya Ardhi ambayo aliianza Juni 24 hadi Julai 15.

Katika operesheni hiyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ikiwa imeambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, watendaji kutoka idara ya ardhi ya wilaya hiyo, wanasheria na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Pwani wamekuwa wakiweka kambi Mapinga kusikiliza migogoro hiyo.

Ni operesheni ambayo imeandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo kwa kushirikiana na watendaji kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Pwani, wataalamu wa sheria kutoka mahakama na Halmashauri ya Bagamoyo.

Okash anasema wamelazimika kuanza katika kata hiyo baadae wataenda Makurunge na Fujayisi kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi.

Okash anasema wameona wawafuate wananchi kwenye maeneo yao yenye migogoro ili kuyatafutia ufumbuzi kwa kushirikiana na wataalamu wa ardhi na wanasheria badala ya kuwasubiri.

Anasema katika baadhi ya maeneo, Kata ya Mapinga kuna mashamba makubwa, nyumba nzuri lakini maeneo wanayoishi hawayamiliki kihalali tofauti na taratibu zinavyoelekeza.

Kadhalika Mkuu huyo wa Wilaya anasema ili kukabiliana na migogoro hiyo pia wameanza kubainisha kampuni zinayojihusisha na kupima na kuuza ardhi katika wilaya hiyo kutokana na baadhi ya kampuni hizo kuhusishwa kuuza maeneo yenye hatimiliki.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salam na Pwani, Shukrani Kyando anasema ameungana na Mkuu huyo wa Wilaya kusikiliza changamoto za masuala ya ardhi na kuyatafutia ufumbuzi.

Kamishna Kyando anasema pia wameitumia operesheni hiyo kutoa ushauri kwa kesi ambazo zipo mahakamani ili wananchi wahakikishe wanatii amri ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

Pia ametoa ushauri kwa wananchi kupima maeneo yao sambamba na kufuata taratibu za umiliki wa ardhi kuepusha migogoro ambayo inatokea kwa kutozingatia taratibu.

Rose Leon ni mmoja wa wananchi waliojitokeza katika operesheni hiyo ambaye anaomba Serikali kufungia kampuni zitakazojihusisha na uuzaji wa ardhi ili kuepuka kazi hiyo kufanywa na kampuni binafsi zinazochangia uwepo kwa migogoro.

Mwinyi Masud, mkazi wa Mingoi amempongeza Mkuu wa Wilaya hiyo kwa kuanzisha operesheni hiyo ambayo anaomba imekuwa msaada kwa walio wengi kutatuliwa migogoro yao sambamba na kupewa ushauri wa kitaalamu kumaliza migogoro hiyo.

Kupita operesheni hiyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo kwa kushirikiana na wataalamu wa ardhi na ofisi ya Kamishna wa Ardhi mkoa wa Pwani wananchi zaidi ya 3,018 walijitokeza kusikilizwa na zaidi ya migogoro 82 imetatuliwa ikiwemo mikubwa ambayo imedumu kwa zaidi ya miaka 10.

Kupitia mkuu huyo wa Wilaya migogoro ambayo ilihitaji suluhu na maridhiano ambayo kwa kipindi kirefu ilisababisha wahusika kwenda mahakamani mara kwa mara hatimaye nayo imetatuliwa kwa makubaliano ya pande mbili zilizokuwa zinahasimiana.

Kufuatia operesheni hiyo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imewabaini baadhi ya vinara wanaotuhumiwa kuhusika katika kuchochea migogoro ya ardhi katika Kata ya Mapinga na maeneo mengine ya wilaya hiyo wakiwemo viongozi wa Serikali na wa chama kwa kuwa mashuhuda wa mauziano ya ardhi zaidi ya mara moja ama kushiriki moja kwa moja kwenye mauziano maeneo yenye migogoro ambapo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Baada ya Operesheni Mapinga Tokomeza Migogoro, Okash anatoa rai kwa wananchi kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi na uuzaji wa ardhi kwa kuwashirikisha wataalamu wa idara ya ardhi wa wilaya hiyo kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Hivi karibuni, aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Slaa naye alifanya ziara katika mkoa wa Pwani na kufanya mkutano wilaya ya Bagamoyo ambapo kupitia kliniki ya ardhi maarufu kama 'Samia Kliniki' alimpongeza Mkuu huyo wa Wilaya kwa jitihada alizofanya kutatua migogoro ya ardhi mingi kwa njia ya suluhu.

Kadhalika Slaa alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha wananchi wenye migogoro kuacha kwenda ofisini kwake na badala yake kutmia kliniki za ardhi kwenye maeneo yao kutafutiwa ufumbuzi wa migogoro yao.

Alisema wananchi wengi wanaoenda ofisini ufumbuzi wa changamoto zao unashindwa kupatikana kwa kuwa watendaji pamoja na makamishna wa ardhi wa maeneo yao hawapo ofisini kwake na kwamba ni lazima watarudishwa kwenye wilaya au mikoa waliyotokea kwa ajili ya utatuzi.

Aliahidi kuendelea kushirikiana na viongozi wa ardhi kuondoa changamoto za migogoro ya ardhi hapa nchini huku akisema watendaji watakaobainika kuhusika kwenye migogoro hatua za kisheria zitachukuliwa.

Waziri mpya aliyeshika nafasi yake, Deogratias Ndenjembi alisema hakuja kutengua Torati akiahidi kuendeleza yote ya mtangulizi wake ikiwemo kliniki za ardhi.

Hata hivyo uhalisia unaonyesha kwamba migogoro ya ardhi katika mkoa wa Pwani inachangiwa na mashamba ambayo hapo awali yaliachwa bila kuendelezwa kwa muda mrefu na hivyo baadhi ya watu kujichukulia sharia mkononi kwa kuwauzia wananchi bila kufuata taratibu.

# Uswisi yamuunga mkono Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Uswisi imesema itashirikiana na Tanzania katika kuchangia Mfuko wa Afya na kusaidia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Hatua hiyo inatajwa kuwa ni kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwahakikishia Watanzania huduma bora za afya kwa wote.

Balozi wa Uswisi anayemaliza muda wake nchini, Didier Chassot, alisema hayo alipokwenda kumuaga Waziri wa Afya Ummy Mwalimu ofisini kwake jijini Dar es Salaam juzi.

Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ulipitishwa kwa kishindo kwa asilimia 100 bungeni jijini Dodoma, Novemba mwaka jana na kuwa sheria.

Akiwa ziarani mkoani Katavi na Rukwa hivi karibuni, Rais Dk. Samia aliwahimiza wakazi wa mikoa hiyo ambao wengi wao wanajishughulisha na kilimo, kuuza mazao yao na fedha wanazopata, wazitumie kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

Alisema Bima ya Afya ni muhimu kwa sababu mwanachama wa mfuko huo anaweza kutibiwa muda wowote na mahali popote pasipo kuhitaji fedha zaidi za matibabu.

Katika mazungumzo yao, Waziri Ummy na Balozi Chassot, walikubaliana kuendelea kushirikiana katika sekta ya afya kwa kuchangia Mfuko wa Afya na kusaidia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ili Watanzania wapate huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

Waziri Ummy aliiomba Serikali ya Uswisi kuiunga mkono na kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa kuchangia Mfuko wa Afya wa pamoja na kusaidia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Kwa upande wake, Balozi Chassot, alimhakikishia Waziri Ummy kwamba Uswisi itaendelea kushirikiana na Tanzania hasa katika upande wa Sekta ya Afya.

"Nitaenda kumweleza mwenzangu anayekuja baada yangu jinsi tulivyokuwa tunashirikiana na Serikali ya Tanzania hasa katika kuchangia Mfuko wa Afya wa pamoja, lakini pia na ombi hilo la kusaidia kufanikisha Bima ya Afya kwa Wote," alisema Balozi Chassot.

Balozi Chassot ameishukuru Tanzania kwa kumpa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake ambapo pia alielezea jinsi Watanzania walivyo wakarimu.

> **Nitaenda kumweleza mwenzangu anayekuja baada yangu jinsi tulivyokuwa tunashirikiana na Serikali ya Tanzania hasa katika kuchangia Mfuko wa Afya wa pamoja, lakini pia na ombi hilo la kusaidia kufanikisha Bima ya Afya kwa Wote**



**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan**

# Dk. Samia kesho kuzindua safari SGR Dar - Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, kesho anatarajiwa kuzindua safari za treni ya kisasa inayotumia umeme (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano cha Shirika la Reli Tanzania (TRC), Jamila Mbarouk, uzinduzi huo utafanyika jijini Dodoma baada ya Rais Dk. Samia kuwasili jijini humo akitokea jijini Dar es Salaam kwa usafiri wa treni hiyo.

Safari za treni ya SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma, zinaanza Julai 25, mwaka huu.

Akizungumzia usafiri wa awali wa treni hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro zilizoanza Juni 14, mwaka huu, alisema hakuna changamoto zozote za kiundeshaji zilizojitokeza hadi sasa.

Kuhusu ratiba ya safari, Jamila alisema treni ya haraka itatoka Dar es Salaam saa 12:00 asubuhi na itatoka Dodoma saa 5:30 asubuhi.

Alisema treni ya kawaida itatoka Dodoma saa 11:30 jioni na itatoka Dar es Salaam saa 12:55 jioni.

Alisema treni ya kawaida inayoishia Morogoro itatoka Dar es Salaam saa 3:30 asubuhi na kuwasili Morogoro saa 5:10 asubuhi, pia itatoka Morogoro saa 3:50 asubuhi na kuwasili Dar es Salaam saa 5:40 asubuhi.



**Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano cha Shirika la Reli Tanzania (TRC), Jamila Mbarouk**



# Kortini akidawa kujeruhi kwa kitako cha bunduki

**Na Racheal Mayanga, DarTu**

MKAZI wa jijini Dar es Salaam, Revin Mwebea (22), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na shitaka la kumjeruhi kwa kitako cha bunduki Omary Athumani (52).

Mshtakiwa huyo alifikishwa katika Mahakama ya Mwanzo Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Mbele ya Hakimu Gladness Njau, hati ya mashitaka iliyosomwa na Karani wa mahakama hiyo, Aurelia Bahati, ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo eneo la Upanga Mtaa wa Mizengo Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam Julai 19, mwaka huu.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alimjeruhi kwa makusudi Athumani kwa kumpiga na kitako cha bunduki sehemu za paji la uso, kisogoni na mdomoni huku akiwa anajua kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo.

Mshtakiwa alirudishwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ambayo ni kuwa na wadhamini wawili waliotakiwa kusaini bondi ya Sh. 300,000 kila mmoja.

Hakimu Njau aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 12, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

# Kesi dhidi ya bosi wa zamani Jatu Public Ltd yaahirishwa

**Na Hidaya Machupa, DarTu**

UPANDE wa Serikali katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jatu Public Limited ya jijini Dar es Salaam, Peter Gasaya, umedai kuwa bado unaendelea na upelelezi.

Wakili wa Serikali, Eva Kassa, alidai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Godfrey Mhini, kesi hiyo ilipotajwa.

Wakili wa Serikali Eva, alidai kuwa, bado upelelezi haujakamilika na kuiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa kwa shauri hilo.

Hakimu alikubaliana na ombi hilo na kuiahirisha hadi Agosti 12, mwaka huu .

Katika kesi hiyo, Gasaya anadaiwa kuwa kati ya Januari mosi, mwaka 2020 na Desemba 31, 2021, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa kama Mkurugenzi wa kampuni hiyo, alijipatia Sh. 5, 139, 865,733 kutoka Saccos ya Jatu kwa njia ya udanganyifu, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Iliendelea kudaiwa kuwa,alijipatia kiasi hicho cha fedha kwa madai ya kuzungusha na kukizalisha kwa kuwekeza katika mazao ya kilimo na kupata faida zaidi, jambo ambalo alifahamu si kweli.


Mashitaka mengine yanayomkabili Gasaya ni kutakatisha fedha hizo zilizokuwa katika akaunti ya Jatu iliyoko benki ya NMB tawi la Temeke kwa kujirushia katika mitandao ya simu (miamala).

Ilizidi kudaiwa kuwa mshtakiwa alifanya hivyo huku akijua kuwa fedha hizo zinatokana na kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

HII NI KERO



## Tuweke uwiano mzuri wa daladala

Ukisimama kwenye kituo cha mabasi (daladala) jijini Dar es Salaam, hususani nyakati za asubuhi na jioni, utagundua kwamba huwa hakuna uwiano wa idadi ya mabasi yanayokwenda sehemu mbalimbali kupitia kituo hicho.

Kwa mfano, ukiwa Mwembe Yanga, utaona mabasi ya kwenda Kariakoo (kutoka Buza) ni mengi, pengine mara tano zaidi ya yale yanayokwenda Mnazi Mmoja na Makumbusho.

Je, wanaosajili mabasi huwa hawaangalii uwiano wa mabasi kwa ruti? Hawatembelei vituo kuangalia hali ilivyo? Kwa nini, kwa mfano, wasajili mabasi 100 kutoka Buza kwenda Kariakoo halafu wakasajili mabasi 20 tu kutoka Buza kwenda Mnazi Mmoja?




MAONI YA MHARIRI

## Tuendelee kutoa maoni Dira ya Mendeleo 2050

MWAKA kesho 2025, Tanzania itakuwa inamaliza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo iliyoandaliwa mwaka 2000. Hatua hiyo maana yake ni kwamba tutaanza utekelezaji wa dira nyingine itakayotupeleka katika kipindi kingine cha miaka 25 kwa maana ya mwaka 2050.

Hakuna ubishi kwamba Dira ya Taifa inayomalizika, imetupa mafanikio mengi na kwa hakika Tanzania ya leo si iliyokuwepo mwaka 2000 kwa takribani kila kitu. Mbali na kuzungumzia ongezeko la miundombinu ya barabara, shule, hospitali, huduma za maji, umeme na kadhalika, yapo mambo ambayo yakitajwa yanasaidia kuonesha namna ambavyo Tanzania imepiga hatua.

Moja ya mambo hayo ni Tanzania kuingia kwenye orodha ya nchi za uchumi wa kipato cha kati cha chini (lower middle-income country) mwaka 2020 baada ya kufikisha wastani wa kipato cha mtu cha dola za Marekani 1,080.

Mafanikio mengine ni wastani wa umri wa kuishi kwa Mtanzania umeongezeka kutoka miaka 52 mwaka 2000 hadi kufikia miaka 66 mwaka 2022.

Takwimu hizo zilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo jijini Arusha Julai 27, 2024 kwenye Kongamano la Kikanda lililokuwa na lengo la kukusanya maoni ya wananchi kuelekea kwenye uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025-2050.

Profesa Mkumbo anasema lengo lilikuwa umri ufike miaka 68 ifikapo mwaka 2025 na kwenye takwimu za sasa wanawake wanaishi umri mkubwa zaidi wa miaka 68 ikilinganishwa na wanaume wanaoishi wastani wa miaka 64.

Lakini kumekuwa pia na kupungua kwa idadi ya vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kutoka vifo 760 katika akina mama 100,000 waliokuwa wanajifungua mwaka 2000 hadi kufikia akina mama 104, na kuvuka lengo la kufikia akina mama 265 ifikapo mwaka 2025.

Kwa sasa maandalizi ya Dira ya Taifa kwa miaka 25 mingine, kwa maana ya kukusanya maoni ya wananchi yanaendelea kutolewa kwa njia mbalimbali.

Kuna mbinu nyingi za kukusanya maoni ikiwa ni pamoja na kushirikisha mikoa ya nchi nzima kupitia makongamano. Tayari yamefanyika makongamano katika mikoa ya Mwanza na Arusha. Makongamano yatakayofuatia ni katika mikoa ya Mbeya, Kigoma, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Unguja na Pemba.

Mbali na makongamano, wananchi wanaweza kuchangia maoni yao kupitia mtandao wa serikali wa DiraPortal.

Ikumbukiwe kwamba mchakato wa kuandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025-2050 unashirikisha wananchi kama njia sahihi ya kujenga mwafaka wa kitaifa kwa kuwa na makubaliano ya pamoja ya kule taifa linapotakiwa kufika.

Na ikumbukwe kwamba hatua hii ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aliyetaka wananchi wote washirikishwe ipasavyo kwenye uandaaji wa dira hiyo ya maendeleo.

Kwa maana hiyo, ni vyema bila kujali itikadi za vyama, za dini wala nini kila Mtanzania ajitahidi kutoa maoni yake katika kupata Tanzania anayoitaka miaka 25 ijayo.


### Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255784122020
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com


Hamid Yassin
JICHO LANGU
0768 888 787

## Wateule msaidieni Rais,msibanange kazi

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amewakumbusha viongozi wanaoapa kuwatumikia wananchi na kutowadhihaki kwani kimsingi ndio waajiri wao.

Rais Samia aliyasema hayo Julai 26, 2024 wakati akiwaapisha viongozi aliowateua hivi karibuni, akiwaonya viongozi wanaotanguliza masilahi yao kazini kuacha mara moja kabla hajawaona.

"Wananchi ndiyo waajiri wetu, kwa hiyo unapokaa kwenye kiti, tai na koti vimekupendeza, fikiri kwamba umefika hapo kwa mamlaka tuliyopewa na wananchi. Niombe sana nendeni mkatumikie wananchi.

"Sitarajii mwende mkadhihaki wananchi au mkawadogoshe, kwa sababu wao ndiyo sababu ya sisi kuwapo hapa, kwa hiyo nendeni mkawatumikie, hakikisheni masilahi yao yanapatikana.

"Na kwa sababu mmeapa niwaibie siri kwamba kiapo kinapiga, ukikiendea upande hakitakuacha, kitakupiga. Ukikidhihaki kitakupiga, kwa hiyo nendeni mkaishi na viapo vyenu," amesisitiza Dk. Samia.

> **Na kwa sababu mmeapa niwaibie siri kwamba kiapo kinapiga, ukikiendea upande hakitakuacha, kitakupiga. Ukikidhihaki kitakupiga, kwa hiyo nendeni mkaishi na viapo vyenu**

Naam; huu ndiyo utawala bora, alichonena Dk. Samia kuwapasulia ukweli wateule wake, unaotokana na mfumo wa uongozi unaozingatia misingi ya uwazi, uwajibikaji, misingi ya haki na sheria kuwawezesha viongozi na watendaji katika utumishi wa umma kufanya kazi kwa ufanisi na uadilifu kwa manufaa ya jamii.

Mfumo huu ukizingatiwa katika uongozi wa jamii au taifa, unasaidia uwajibikaji wa kweli katika kutekeleza majukumu yanayopangiwa hawa viongozi wetu.

Hapa nia hasa ni kuhakikisha vyombo vyote vya mamlaka vinatenda kazi kwa kuzingatia misingi ya haki na usawa, na kuwaheshimu wananchi wanapohitaji huduma kutoka kwa hawa waliokabidhiwa dhamana ya kumsaidia kazi Mheshimiwa Rais.

Ili kutekeleza dhana ya utawala bora mambo yafuatayo lazima yazingatiwe, ambayo ni pamoja na matumizi sahihi ya dola, matumizi mazuri ya madaraka, kujua na kutambua madaraka waliyonayo na matumizi yake na madaraka yanatumika kulingana na mipaka iliyowekwa na Katiba na Sheria.

Thamani na heshima ya kiongozi kwa anaowaongoza ipo katika uwezo wake katika kupambanua mambo kimkakati, kuwaelewesha na kuwajengea hamasa anaowaongoza ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Siyo kiongozi anaapa huku akiwa kashika kitabu kitakatifu cha dini anayoiabudu, lakini akili yake inakuwa haipo pale, bali anawaza jinsi atakavyofaidi keki ya taifa na jinsi atakavyowadhibiti watakaojaribu kumtilia kitumbua chake mchanga!

Kiongozi badala ya kuwaza jinsi atakavyoyakabili na kuyapatia ufumbuzi majukumu aliyokabidhiwa, yeye anaanza kujenga safu za matabaka kazini kwake ili awagawe na kuwatawala atakavyo yeye! Huyo hatufai hata kidogo.

Kiongozi anafika mapema ofisini, lakini kwa sababu anazozijua yeye anawaambia wasaidizi wake; "Leo sitaki wageni."

Katika hali ya kawaida, zipo siku kweli viongozi wanaweza wakawa wanatimiza majukumu ya ndani ya ofisi, lakini hii kwa viongozi wengi imekuwa ni tabia yao ya kila siku kazini!

Hebu tuache kubananga kazi, tumsaidie Mhesimiwa Rais Dk. Samia kutimiza ahadi za Ilani za Chama chake kuwaletea maendeleo wananchi.

Kumbuka, uongozi ni dhamana. Kazi ya kiongozi ni kuwatumikia wananchi na kero zote za wananchi ni mzigo wa kiongozi huyo.



# Hatari za kiafya za kuweka kope bandia

**Na Mwandishi Wetu**

KOPE za asili hufanya kazi muhimu, hulinda macho kwa kuelekeza hewa mbali na mboni ya jicho na kumfanya mtu kupepesa, hatua ambayo pia huhakikisha kwamba macho yana majimaji vizuri.

Kope bandia hushikanishwa na kila kope asili, moja kwa moja.

Kope hizi huunganishwa na gundi ambayo inaweza kusababisha matatizo.

Wataalamu wengi wa vipodozi hufanya jaribio la awali la kiraka cha kope bandia kwenye eneo fulani la mwili, kwa kawaida kwenye mkono au nyuma ya sikio, ili kuangalia mizio ya gundi; hata hivyo, hata ikiwa hakuna athari ya mzio, kemikali katika gundi, inaweza kuwasha eneo la jicho na uzito wa gundi yenyewe inaweza kusababisha muwasho kwenye kope.

Kumekuwa na ripoti za watu ambao kope zao zimeshikamana kwa sababu ya matumizi ya kope bandia.

Kwa mujibu wa utafiti mmoja, zaidi ya asilimia 60 ya wanawake waliripoti changamoto ya keratoconjunctivitis, hali ya jicho inayohusisha kuvimba kwa kornea na kiwambo cha jicho kwa wakati mmoja, baada ya gundi ya kope bandia kugusa macho yao.

Utafiti huo huo uligundua kuwa asilimia 40 ya wanawake, walipata athari ya mzio kwa sababu ya gundi.

**Gundi inayosababisha saratani**

Kumekuwa na nyakati ambapo gundi ya kucha, ambayo ina nguvu zaidi, huuzwa kama gundi ya kope.







Katika mojawapo ya matukio ya kushtua ya utumiaji usiofaa, kope za mwanamke ziliachwa zikiwa zimeshikamana pamoja baada ya kuweka kope bandia kwa kutumia gundi kali.

Gundi ya kope inaweza kusababisha hatari kadhaa za afya.

Utafiti mmoja ulichanganua viambata 37 vya kibiashara na kitaalamu na kugundua uwepo wa formaldehyde, kemikali inayojulikana kusababisha saratani.

Uchambuzi huo uligundua kuwa asilimia 75 ya viambata 20 vya kitaalamu vilivyojaribiwa, vilitoa formaldehyde na gundi nne kati ya 17 za kibiashara pia zilikuwa na kemikali hiyo.

BBC.



Na Ahmed Rage Simu: 0717 658574

# Mtambue mteja stahiki na unayemlenga-2

KUUNDA simulizi za mteja stahiki: Kuandika hadithi za kina kuhusu maisha ya mteja wako stahiki, ikijumuisha malengo yao, vikwazo wanavyokutana navyo na jinsi bidhaa/huduma yako inaweza kuwasaidia.

Hadithi hizi zinaweza kusaidia kikosi kazi chako cha mauzo na maendeleo ya bidhaa kuelewa vizuri zaidi wateja na jinsi ya kuwatumikia.


**5. KUWEKA MIKAKATI YA KUWAFIKIA WATEJA BAADA YA KUTAMBUA WATEJA STAHIKI NA WALENGWA, NI MUHIMU KUUNDA MIKAKATI YA KUWAFIKIA. HII INAWEZA KUFANYWA KUPITIA:**

**a. Uuzaji wa kidijitali**

Kutumia zana na njia za kidijitali kama vile uwezo kupatikana mtandaoni kwa urahisi (UKUMU), matangazo ya kulipwa, na mitandao ya kijamii ili kuwafikia wateja walengwankwa ufanisi zaidi. UKUMU inasaidia kuboresha nafasi ya tovuti yako kwenye injini za utafutaji, huku matangazo ya kulipwa na kampeni za mitandao ya kijamii zikilenga wateja maalum kwa kutumia vigezo vya kidemografia na tabia.

**b. Masoko Maudhui**

Kuunda na kusambaza maudhui yenye thamani ambayo yanavutia na kuelimisha, kutoa habari na kuburudisha wateja walengwa. Hii inaweza kujumuisha blog, picha za video, datapicha (inforgraphics) na machapisho ya mitandao ya kijamii. Kwa mfano, kampuni inayouza vifaa vya mazoezi, inaweza kuunda maudhui yanayohusu faida za mazoezi na jinsi ya kutumia vifaa hivyo kwa ufanisi.



> **Aidha, kutambua mteja stahiki na anayelengwa, ni msingi wa mafanikio ya biashara yoyote. Kwa kutumia njia bora za kutathmini soko, biashara zinaweza kuelewa vizuri mahitaji na matarajio ya wateja wao na hivyo kuunda mikakati madhubuti ya kuwafikia na kuwahudumia. Hatua hizi siyo tu zinasaidia kuongeza mapato, bali pia zinaboresha uhusiano na wateja na kuleta ufanisi wa muda mrefu kwa biashara. Kwa kuwa na uelewa mzuri wa soko lako na wateja wako, unaweza kufanya maamuzi sahihi na kuboresha nafasi yako ya kufanikiwa katika soko lenye ushindani.**

**c. Masoko kupitia barua pepe**

Kutumia kampeni za barua pepe mahsusi kwa mteja ili kuwafikia wateja walengwa moja kwa moja.

Hii inasaidia katika kujenga uhusiano wa muda mrefu na wateja na kuongeza mauzo. Barua pepe zinaweza kujumuisha ofa maalum, habari kuhusu bidhaa mpya, au maudhui yanayowafaa wateja kulingana na tabia zao za ununuzi.

**6. KUFUATILIA NA KUPIMA MATOKEO**

Ni muhimu kufuatilia na kupima matokeo ya mikakati yako ya uuzaji ili kuona kama zinafanya kazi ipasavyo. Hii inaweza kujumuisha kutumia zana za uchambuzi wa tovuti, ufuatiliaji wa kampeni za barua pepe, na utafiti wa kuridhika kwa wateja.

Kupima matokeo kunaweza kusaidia kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa na kufanya mabadiliko muhimu ili kufikia malengo ya biashara yako.

**7. KUJIFUNZA NA KUBORESHA**

Biashara inapaswa kuwa na uwezo wa kujifunza kutokana na matokeo ya utafiti na mikakati iliyotekelezwa.

Hii inamaanisha kuwa tayari kufanya mabadiliko kulingana na maoni ya wateja na data zilizokusanywa. Endelea kuboresha mikakati yako na kujifunza kutokana na mafanikio na makosa yaliyopita.

Aidha, kutambua mteja stahiki na anayelengwa, ni msingi wa mafanikio ya biashara yoyote. Kwa kutumia njia bora za kutathmini soko, biashara zinaweza kuelewa vizuri mahitaji na matarajio ya wateja wao na hivyo kuunda mikakati madhubuti ya kuwafikia na kuwahudumia.

Hatua hizi siyo tu zinasaidia kuongeza mapato, bali pia zinaboresha uhusiano na wateja na kuleta ufanisi wa muda mrefu kwa biashara. Kwa kuwa na uelewa mzuri wa soko lako na wateja wako, unaweza kufanya maamuzi sahihi na kuboresha nafasi yako ya kufanikiwa katika soko lenye ushindani.

Kwa kuzingatia hatua hizi zote, biashara yoyote inaweza kuwa na uhakika wa kujenga msingi imara kwa ajili ya ukuaji endelevu na mafanikio ya muda mrefu.

**Utafiti wa soko**

Uchambuzi wa tabia za wateja, utambuzi wa soko lengwa, uundaji wa sifa za mteja stahiki, kuweka mikakati ya kuwafikia wateja, kufuatilia matokeo na kujifunza na kuboresha, ni nguzo muhimu za safari ya kuelekea mafanikio ya biashara yoyote ile.

*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA **Jungu Kuu** Jumatano Julai 31 - Agosti 6, 2024

UTALII
AFYA
JAMII

# Vigingi vinavyomsubiri Lissu nia yake ya urais

Jarida hili haliuzwi

UK. 12 & 13

UK. 10




UK. 11

# Mpango wa kunusuru kaya maskini ulivyomnusuru Regina

**Na Mwandishi Wetu, Bagamoyo**

NI miaka kumi imepita tangu Regina Masatya (49) aingizwe kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Katika makala haya, Regina Mkazi wa Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani anaeleza hali aliyokuwa nayo mwaka 2014 wakati anaingia kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini na hali yake ya sasa.

"Mimi na mume wangu tulikuwa tunaishi Kahama. Mwaka 2000 wakati huo tukiwa na watoto wawili, tukaamua kuhamia hapa Mapinga kujaribu maisha ya huku Pwani. Kwa kweli tuliishi maisha ya furaha kwa kipindi cha takribani miaka minane kabla ya maisha kuanza kuwa magumu na maelewano ndani ya nyumba kuwa mabaya sana," anasema.

Anasema baadaye ndoa yao ilivunjika, mume wake akamwacha na kwenda kuanza maisha mapya katika eneo la Zinga. Yeye akabaki na watoto wote wanne waliokuwa nao wakati huo.

"Mume wangu alikwenda kuanza maisha kwingine na kuniachia familia ya watoto wanne katika nyumba ya kupanga, nikiwa na vyumba viwili nilivyotakiwa kuvilipia kodi kila mwezi. Yaani fikiria nina watoto wanne, sina kazi lakini pia ninatakiwa kulipa kodi ya pango. Hali ilikuwa ngumu sana," anasema.

Anasema mazingira aliyojikuta yumo, yalimlazimisha kuingia kwenye kufanya vibarua vya kulima mashamba ya watu ambayo ni kazi ya msimu, uchimbaji wa mitaro ya mabomba na kuchimba visiki ili aweze kujikimu yeye na familia kwani mumewe alimsusia kabisa familia.

Anasema aliendelea na kazi hizo na wakati mwingine familia yake ililazimika kupata mlo mmoja kwa siku pale ambapo amepata kibarua chenye malipo finyu.

"Sikuwa nimezoea maisha ya kula mlo mmoja lakini wakati ulifika, kuna siku fedha ninayopata ni ndogo haimudu kununua chakula cha milo mitatu. Kwa kuwa nina fedha ya kukidhi mlo mmoja tu, nalazimika kusubiri watoto wote watoke shule ndio tunakula," anasema.

Anasema katika kipindi hicho alikuwa mara nyingi akifanya kazi ambazo zimezoeleka kuwa ni za wanaume, kazi za misuli lakini alikuwa hana namna kwani asipotoka basi watoto wanalala na njaa.

"Hali ilikuwa ngumu. Hata kama ni ninaumwa ninajikongoja. Nisipotoka kusaka vibarua watoto hawali... Sitasahau nilivyofanya kazi za kuchimba mtaro wa kuwekea mabomba ya maji. Ilikuwa ni kazi ngumu kwangu lakini sikuwa na mbadala," anasema.

Anasema vibarua kwenye mashamba ambavyo ni vya msimu mfupi vilikuwa na ahueni ya malipo kwani alikuwa anapata kati ya shilingi 10,000 na shilingi 15,000 kwa siku lakini kwa upande wa kuchimba mitaro, licha ya kazi hiyo kuwa ngumu, aliambulia shilingi 2,100.

Anasema si kazi ya visiki na mitaro pekee alizolazimika kufanya bali pia kuchoma mkaa alifanya ili apate chochote, mkono wake na wanawe uende kinywani na pia apate fedha kwa ajili ya matumizi ya watoto wake shuleni.

Anasema alikuwa anatamani kufanya ujasiriamali lakini kikwazo kikawa ni mahala pa kupata mtaji.

Anasema pamoja na kupambana na vibarua bado alikosa kutunza fedha ya kulipa kodi ya nyumba, hivyo akajikuta anadaiwa kodi ya miezi sita hadi pale mwenyekiti wa serikali ya mtaa wake alipomtafuta mume wake asaidie kulipia kodi hiyo.

"Mwenye nyumba alikuwa amechachamaa anataka kunifukuza kwenye nyumba yake baada ya kukaa kwa muda mrefu bila kulipa kodi. Kumbuka ninadaiwa kodi wakati kuna siku ninakosa chakula na wanangu. Ninashukuru majirani walikuwa wanajua hali yangu, walikuwa wananisaidia nikikwama sana," anasema.

Anaendelea kusimulia, "Mwaka 2014 watu wa TASAF walipotutembelea walinikuta niko kwenye kipindi kigumu, nikiendelea kufanya kazi ngumu ili kujikimu. Waliponitembelea nyumbani walinikuta nikiwa ninatoka kibaruani. Hali walioiona haikuwa vigumu kukubaliana na taarifa walizopewa kuhusu maisha yangu," anasema.

Anasema baada ya kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini alinufaika kwa kupata ruzuku kila mwezi ambayo ilimsaidia kununua chakula sambamba na mahitaji ya vifaa vya shule kwa watoto wake.

Anasema kutokana na namna alivyoitumia ruzuku hiyo, ndani ya miaka kumi tangu aingizwe kwenye mpango ilimsaidia kuimarika kwa kufanya shughuli ndogondogo za ujasiriamali na hatimaye kuwa mmoja wa waliotoka kwenye mpango ili kupisha wengine nao wanufaike na mpango huo.

Regina anasema mwanzoni mwa mwaka huu alipatiwa ruzuku ya Sh. 500,000 baada ya kujitoa kwenye mpango ambazo amezitumia kuendeleza shughuli za kilimo kwa kukodi mashamba kwa ajili ya kulima viazi na mpunga.

"Ruzuku za kila mwezi ziliniimarisha katika shughuli za kilimo, pia nimefanikiwa kununua kiwanja na sasa natafuta fedha kwa ajili ya kujenga. Kupitia kilimo ninaamini nitafikia malengo niliyojiwekea," anasema.

Kwa sasa Regina anasema amepeleka maombi yake ya kupata jenereta kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kipindi cha kiangazi kwa viongozi wa TASAF ambao tayari wamemtembelea kwenye miradi yake ya kilimo. Hatua hiyo anaamini itamwezesha kulima zaidi ya mara moja kwa mwaka bila kulazimika kusubiri mvua .

Mkurugenzi wa Uratibu kutoka TASAF, Haika Shayo ambaye alimtembelea mnufaika huyo akiongozana na watendaji wa mfuko pamoja na mmoja wa wadau wa maendeleo anasema wapo wanufaika wamekuwa na matokeo chanya kupitia ruzuku wanazopata ikiwa ni pamoja na Regina.

Shayo anasema Regina ni kati wanufaika wa mpango katika Wilaya ya Bagamoyo ambao walitembelewa na watendaji hao kuona maendeleo yao na haja ya kuwasaidia zaidi.

Anasema lengo lao hasa ni kuona chochote kilichoanzishwa kwenye mpango kinakuwa endelevu kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa.

Akizungumzia kuhusiana na walengwa ambao wameanza kutoka kwenye mpango, Shayo anasema wapo ambao tayari wamejiimarisha na kupewa ruzuku kuendeleza miradi waliyoianzisha na kutoa nafasi kwa wengine kutoka kaya masikini kuingizwa kwenye mradi.

Mmoja wa wadau wa Maendeleo, Nancy Kataraihya anasema amefurahishwa na namna wanufaika walivyoonesha mafanikio kupitia mpango huo wa kunusuru kaya maskini.

Mratibu wa TASAF wa Mkoa wa Pwani, Roseline Kimaro amesema mkoa huo unaendeleza jukumu la kusimamia, kuratibu na kutekeleza kazi zilizopangwa kwa walengwa wa mpango.

Roseline anasema wanufaika wengi wamekuwa na mabadiliko ya kimaisha hususani uwezo wa kiuchumi ukilinganishwa na kipindi walivyokuwa wanaingizwa kwenye mpango.

Kwa mujibu wa Kimaro wanufaika 4,451 wametoka kwenye mpango kwa nyakati tofauti na kwa sasa ni kaya 18,487 ambazo zimebaki kwenye mpango huo wa kunusu kaya masikini.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Jalala Sammatta amesema yapo makundi mawili ambayo yametoka kwenye mpango likiwemo kundi lililotoka baada ya kupewa ruzuku ya uzalishaji na waliotoka baada ya kufanyiwa tathmini ambao wote waliingia kwenye mpango mwaka 2014.



# Wagombea uongozi TLS waahidi makubwa



Wagombea wakiwa kwenye mdahalo.

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI za Uchaguzi Mkuu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), ambao unatarajiwa kufanyika keshokutwa Agosti 2 mwaka huu zinaendelea kupamba moto kwa kila mgombea kunadi sera zake iwapo atachaguliwa kukiongoza chama hicho kwa muhula wa miaka mitatu.

Uchaguzi huo utafanyika kwa kutanguliwa na Mkutano Mkuu wa mwaka wa TLS kuanzia tarehe moja Agosti mwaka huu mkoani Dodoma na tayari wagombea wameshaanza kunadi sera zao wakitaja mambo watakayoyafanya wakishinda.

### SAKATA LA MWABUKUSI

Uchaguzi mkuu huo umekuwa maarufu siku za karibuni baada ya mmoja wa waliooneshа nia ya kugombea nafasi ya Rais wa TLS, Wakili Boniface Mwabukusi kuondolewa kwenye kinyanganyiro hicho na Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi ya chama hicho kwa madai ya kukiuka baadhi ya kanuni za fani hiyo.

Hata hivyo, Wakili Mwabukusi atagombea nafasi hiyo baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutengua uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi ya TLS iliyomwengua kugombea nafasi hiyo Julai 5 mwaka huu.

Mwabukusi ameshinda baada ya kuwakilishwa mahakamani na jopo la mawakili 29 na kutoa hoja mbili kupinga uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi akieleza kuwa haikuwa na mamlaka ya kumwengua kugombea baada ya kupitishwa na kwamba hakupewa haki yake ya kusikilizwa.

### WAGOMBEA SITA

Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ni taasisi muhimu inayochangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha mfumo wa sheria na haki nchini Tanzania na kwa mwaka huu wagombea wa nafasi ya urais kwenye uchaguzi huo wa mwaka huu watakuwa sita, Mwabukusi, Emmanuel Muga, Ibrahim Bendera, Paul Kaunda, Revocatus Kuuli na Sweetbert Nkuba.

Baadhi ya wananchi wanakiona chama hicho kama chama cha harakati zaidi kutokana na misuguano yake ya mara kwa mara baina yake na serikali huku wengine wakikiona kama chama cha kitaaluma kilichotoa mchango katika kuiendeleza taaaluma ya sheria na kutetea wanachama wake pale wanapoguswa.

### NITALETA UZOEFU WA KIMATAIFA

Mmoja wa wagombea nafasi hiyo, Wakili Paul Kaunda amejinadi kuwa yeye si mgeni kwenye uongozi kwani amefanyakazi kwa miaka 10 katika maeneo mbalimbali ya sheria hasa sheria za jina na madai na ni mdau mkubwa sana kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda yaani akili mnemba (AI).

Anasema kwamba yeye pia siyo mgeni wa kuongoza taasisi kama TLS kwani 2019 -2020 alipata bahati ya kutumika kama Mjumbe wa Baraza la Uongozi na Mjumbe wa Kamati ya Sheria na Katiba ya TLS kwa miaka mitano.

Kaunda anasema kutokana na umahiri wake alionekana na akaaminiwa na Chama cha Mawakili wa Afrika kutumika kama Makamu wa Rais wa Pan African Lawyers 2018-2021 na kwamba anaamua kugombea kwa sababu ataleta uzoefu wa mambo mazuri ambayo ameyapata ndani ya chama hicho.

"Nimedhamiria kuleta heshima kwa TLS na nyote ni mashahidi kwamba heshima ya chama hiki imeshuka sana kwa hiyo nitakwenda kurejesha heshima hasa sisi mawakili tunapowawakilisha wateja wetu wakiwa polisi, magereza na mahakamani," anasema.

### NITAPAMBANA NA MAWAKILI VISHOKA

Mgombea mwingine, Sweetbert Nkuba naye anasema ana uzoefu wa muda mrefu wa uongozi katika ngazi mbalimbali na hivyo anaomba achaguliwe kwenye nafasi hiyo ili afanikishe vipaumbele vitano ikiwemo kuwaunganisha wanachama wa TLS na kuhakikisha maslahi ya kiuchumi ya wanachana wa chama hicho yanazingatiwa.

"Nikichaguliwa nitahakikisha wanachama wote wa TLS wanakuwa na bima ya afya, bima ya maisha, nitaanzisha kituo cha malezi kwa wanachama wanaochipukia, kuimarisha uhusiano baina ya wanachama wa TLS, Serikali, mahakama na jamii kwa ujumla," anasema Nkuba

Anasema jambo lingine linalomsukuma kuwania nafasi hiyo ni kupambana na mawakili vishoka ambao hawana sifa ya kufanya kazi hiyo lakini wamekuwa wakisimama mahakamani hivyo kuwanyima nafasi mawakili ambao wamesomea.

Anasema kuna baadhi ya sheria zinazotungwa na seriali na matamko na miongozo inayowanyima mawakili kazi na kukataa kupokea nyaraka ambazo zimesainiwa na kuwekwa mihuri na mawakili wa kujitegemea.

### MAWAKILI WAPYA WATAPETA

Naye Ibrahim Bendera anasema amefanya kazi ya uwakili kwa miaka 18 upande wa Tanzania Bara na miaka 19 kwa upande wa Zanzibar hivyo amejipima na kuona anatosha kuongoza chama hicho hasa wakati huu ambapo rais wa chama hicho ataongoza kwa miaka mitatu badala ya mwaka mmoja.

"Zamani Rais alikuwa anahudumu kwa mwaka mmoja, sasa kwa mwaka mmoja siyo rahisi kuleta mabadiliko kwa hiyo baada ya mabadiliko na kuweka ukomo wa miaka mitatu nimeona nitapata nafasi ya kulieleza Baraza la Uongozi maoni yangu na mpango mkakati wa TLS unaisha mwaka huu kwa hiyo nitaweka msukumo wa kutengeneza mpya," anasema.

Anaendelea: "Nimekuwa mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya TLS kwa miaka minane. Nimeona wapi kwenye shida kwa hiyo nitasimama kurejesha maadili ya uwakili na nitawaunganisha mawakili wapya na wale wa zamani ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi."

Anasema mawakili wapya 555 walioapishwa mwaka huu wana madeni mengi kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), hivyo moja ya majukumu yake itakuwa kuwawekea mazingira mazuri ya kujeresha mikopo kwa kupata kazi za uwakili.

"Hawa mawakili wapya wengine wanadaiwa milioni 20, wengine milioni 30 sasa hawawezi kurejesha bila kusaidiwa kwa kuwekewa mazingira mazuri hawa vijana wapya," anasema wakili Ibrahim

Anasema kwa mwaka TLS yenye wanachama 12,000 inapata wastani wa shilingi bilioni 1.2 na inalipa mishahara inayofikia shilingi milioni 80 kwa mwezi hivyo akichaguliwa atahakikisha anapunguza gharama za matumizi na kuwawekea mazingira mazuri mawakili vijana waweze kupata uzoefu.

### NITABORESHA MASLAHI YA MAWAKILI

Revocatus Kuuli kwa upande wake, anasema yeye amekuwa wakili kwa miaka 13 Tanzania Bara na wakili Zanzibar kwa miaka minne na kwamba katika mawakili 13 waliosajiliwa na Mahakama ya Arika iliyoko mkoani Arusha yeye ni miongoni mwao.

Anasema anafanya kazi pia kwenye Mahakama ya Umoja wa Mataifa ya IRMCT yenye Makao yake Makuu Geneva Uswis na Arusha Tanzania na kwamba ametumikia nafasi mbalimbali serikali na ngazi yake ya mwisho serikalini alikuwa Principle Officer, Wizara ya Katiba na Sheria.

"Nawania nafasi ya urais wa TLS kutaka kutekeleza yale yaliyoko kwenye section 4 ya chama chetu ambayo ni kuboresha maslahi ya wanachama, kuwalinda mawakili na kuwaendeleza kitaaluma. Kwa hiyo nikipata nafasi nitafanya mambo makubwa ambayo kwa miaka iliyopita yalionekana magumu," anasema.

### NINAJUA NINI KIFANYIKE TLS

Naye Wakili Emmanuel Muga anasema amekuwa wakili kwa miaka 12, hivyo amejipima na kuona kuwa anaweza kumudu majukumu ya kuwasimamia mawakili wenzake kama atachaguliwa kushika nafasi hiyo kwenye uchaguzi ujao.

Anasema amekuwa mwenyekiti wa TLS Mkoa wa Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka miwili akianzia 2019 mpaka 2021 na kwamba fursa hiyo ndiyo ilimpa nafasi ya kuwafahamu mawakili na mahitaji yao na nini kifanyike ili chama hicho kiweze kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

"Nikiwa Mwenyekiti wa TLS Mkoa wa Dar es Salaam nilifanikiwa kuunda kamati nane na zilileta mageuzi makubwa sana tunayoyaona kwa Chapter ya chama chetu hapa Dar es Salaam kwa hiyo mafanikio haya ndiyo yamenifanya nione ninaweza kuongoza chama hiki kwa ubora," anasema.

*Inaendelea uk. 18*



# Vigingi vinavyomsubiri Lissu nia yake ya urais

**Na Hamid Yassin**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu mapema kabisa ametangaza nia ya kugombea urais wa Tanzania kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Akiongea mwishoni mwa wiki, Lissu ameweka wazi kuwa nia yake ipo palepale kama alivyogombea urais mwaka 2020 na mwakani atatia timu uwanjani!

Akiongea Julai 26, 2024 muda mfupi baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere Jijini Dar es Salaam akitokea nje ya nchi alikokwenda 'kupumzika', Lissu alinena; "Nilipokuwa namkabili Magufuli (John Pombe) mwaka 2020 nilikuwa na miaka 52 mwaka ujao nitakuwa na miaka 57, kwa hiyo haiwezi ikawa nina nguvu zilezile lakini nguvu ya hoja, na msimamo wa kisiasa na uaminifu kwa Watanzania bado upo palepale."

Lissu aliyepata kura 1,933,271 sawa na asilimia 13.04 dhidi ya zile alizopata hayati Dk. John Pombe Magufuli 12,516,252 sawa na asilimia 84.40, anasema nia yake ya kugombea urais mwaka 2025 ipo palepale, na anasisitiza ataitikia wito wa Watanzania sambamba na chama chake cha Chadema kama kitampitisha kugombea.

Ni jambo zuri kwa Lissu kutangaza nia yake mapema kama alivyofanya ili aanze kupima upepo kutoka pande mbalimbali kama maji aliyoyavulia nguo atamudu kuyaoga!

**RAIS ANAYEPUMZIKA ULAYA**

Sio siri, Lissu atakabiliana na upinzani mkali kutoka ndani na nje ya chama chake kutokana na maadui wengi aliowatengeneza yeye mwenyewe. Hata hilo la kwamba ametangaza nia akitokea Ulaya kupumzika kwa wiki tatu linafikirisha sana, kwamba atakuwa Rais wa aina gani kwani wangetegemea awe ametokea kupumzika nyumbani kwao Ikungi, Singida kwa ndugu zake wa damu!

Tangu alipotimkia Ulaya kwa ajili ya matibabu, amenogewa na amekuwa ni mtu wa kupenda kwenda Ulaya na kupenda pia mambo yao yakiwemo yakiwemo ya kupigia debe ushoga.

Nafuu safari hii amesema kweli kwamba alikwenda kupumzika Ulaya, kwani baada ya kubwagwa kwenye uchaguzi mkuu uliopita, alikimbia Ulaya baada kuomba hifadhi kwenye ubalozi wa Ujerumani jijini Dar es Salaam akiipakazia serikali kwamba eti inamwinda kumuua!

Yaani serikali ya chama tawala imekupa ulinzi wakati wote wa kampeni halafu ije ikuue baada ya mgombea wake kukushinda kwa kishindo!

**MBOWE NAYE ANAUTAKA!**

Kwa hali ya kawaida unaweza kudhani kigingi kwa Lissu kitakuwa Chama Cha Mapinduzi pekee, la hasha! Utakuwa umekosea sana; mtihani wa kwanza wa mwanasiasa huyu ataupata kutoka ndani ya chama chake Chadema.

Duru za kisiasa zinaonyesha Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe naye anataka kujaribu bahati yake ya kugombea urais wa Tanzania kwa mara ya pili baada ya kuanguka vibaya mwaka 2005 mbele ya Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete.

Hivi sasa Chadema kuna kambi mbili, ile ya 'Timu Mbowe' na ya 'Wafia Lissu'! Usidhani kambi hizi zimeibuka kwa ajili ya uchaguzi wa ndani tu wa chama hicho, hapana. Hii ngoma ni hadi kumpata mgombea wao wa urais



mwakani!

Mbowe keshaapa kwamba, lazima atetee nafasi yake ya uenyekiti wa Chadema na mwakani iwe isiwe, yeye ndiye atapeperusha bendera za chama hicho kwenye kugombea urais. Patamu hapo!

Naamini Lissu analijua hili, ndiyo maana amekuwa akimpiga vijembe bosi wake huyo katika patashika za uchaguzi wao wa ndani kwamba, amemwaga fedha chafu kuhakikisha watu wake anaowataka wanashinda kwenye chaguzi zote za ngazi ya chini zikiwemo zile muhimu za ngazi ya kanda zote za chama hicho.

Hii ndiyo sababu ya aliyekuwa kiongozi muhimu wa chama hicho, Mchungaji Peter Msigwa kutimkia Chama tawala, CCM, baada ya kupigwa nyundo ya uhakika ya siasa kule kwenye uchaguzi wa Kanda ya Nyanda ya Juu na 'Timu Mbowe'!

Kule alitumwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama hicho, Benson Kigaila kwenda 'kumshughulikia' Mchungaji na kwa kweli lengo lilifanikiwa kwa wapigakura watatu wa kambi ya Msigwa kuzuiwa kushiriki uchaguzi ule dakika za mwisho na hatimaye chaguo lao, Joseph Mbilinyi alishinda kwa tafauti ya kura moja tu!

Hapa ujue huyu Msigwa alikuwa 'Timu Lissu', hivyo hali ile ilizidisha chuki ya Makamu Mwenyekiti kwa Mwenyekiti wake na kuanza kuhoji fedha zinazotumika kama rushwa kwenye chaguzi hizo za ndani za Chadema zinatoka wapi?

Lissu anajua wazi kwamba hawa viongozi wanaochaguliwa kwa mlango wa uani ni kwa ajili ya kwenda kutumika kumrudisha Mbowe kwenye kiti chake cha enzi sambamba na kupitisha jina lake kuwa mgombea wao wa urais katika Uchaguzi Mkuu wa nchi hapo mwakani.

Sijui Lissu anapata wapi jeuri ya kutangaza nia ya kugombea urais mapema hivi! Maana naamini atadhibitiwa pande zote kwa sababu watu wengi wa kambi yake wamepukutishwa kwenye chaguzi hizi za ngazi ya chini ya chama hicho.

Tunaambiwa hiki ni chama cha demokrasia, lakini kamwe siamini kama demokrasia itaachwa itamalaki ili impe mwanya wa Lissu kutimiza ndoto zake za kuwania urais kwa mara nyingine.

Kama kule ngazi ya chini watu wake wote wamechinjiwa baharini, huku ngazi ya chaguzi za juu Lissu ataponaje? Ajiandae tu kisaikolojia hali ni tete sana kwa upande wake!

### YA SLAA YANAWEZA KUMKUTA

Tukumbuke pia yaliyomkuta Padri Wilbrod Slaa katika uchaguzi wa mwaka 2015. Alikuwa amejianda kugombea tena urais kwa takribani miaka mitano baada ya uchaguzi wa 2010 lakini ghafla upepo ukabadilika. Mbowe na genge wakamtaka Edward Lowassa (RIP) kwa udi na uvumba ambaye waliamini atawaondolea gundi la kutoingia Ikulu.

Kutokana na chama chao kupoteza mwelekeo na mvuto, bila shaka mwanasiasa kutoka CCM akienda huko Chadema, mwenye chama chake, Mbowe, atampa nafasi hiyo bila kujali makunyanzi ya mtu.

### KAMBI YA UPINZANI KUTOMUUNGA MKONO

Kama Lissu atafanikiwa kupenya kwenye tundu la sindano na kupitishwa kuwa mgombea wa Chadema hapo mwakani, ngoma itakuwa haijaisha, kwani atakutana na kigingi cha kingine kutoka vyama vingine vya upinzani vya hapa nchini.

Lissu amejenga uhusiano mbaya na vyama vingine kutokana na tabia yake ya kuvidharau na kuzua sitofahamu mara kwa mara na viongozi wa vyama hivyo ambavyo vingeweza kumuunga mkono kwenye azma yake hiyo ya kwenda Ikulu ya nchi.

Ni hivi karibuni tu vyama vya upinzani 11 vilikutana kule Zanzibar na kulaani vikali kauli zake za kibaguzi dhidi ya kiongozi wa taifa hili, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Viongozi wale wa vyama 11 vya siasa walilaani vikali kauli za Lissu ambazo walidai kuwa ni za kebehi na uchochezi zinazolenga kuleta ubaguzi kwa Watanzania kupitia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Akitoa wasilisho la pamoja la viongozi wa vyama hivyo 11 vya siasa juu ya kauli hizo, Mwenyekiti wa Chama cha ADA TADEA, Juma Ali Khatib alisema kauli zilizotolewa na Lissu ni kauli za kibaguzi ambapo waliziomba mamlaka husika ikiwemo Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na vyombo vingine kuangalia kwa makini hatua za kuchukua kwa kiongozi huyo na chama chake.

"Sisi Vyama 11 vya siasa hatuungi mkono kauli zako Tundu Lisu na tunazilaani. Matamshi yako ya kibaguzi kwa kuonesha wazi watu wa upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawana haki ya kufanya kazi upande mwingine huu ni ubaguzi, uchochezi na kuonesha wazi amefilisika kimawazo, kifikra na kisiasa na kutafuta kiki za kisiasa," alisema Khatib.

Kwa msingi huu alioonesha Makamu Mwenyekiti wa Chadema ni dhahiri anawaambia wananchi kwamba yeye ni mbinafsi, mwenye uchu wa madaraka, mchonganishi, mfitinishaji na mwenye dhamira ovu kwa Muungano wetu," aliongeza Khatibu.

"Tunavitaka vyombo vya ulinzi na usalama nchini, pamoja na msajili wa vyama vya siasa kufanya uchunguzi wa kina juu ya kauli anazozitoa ndugu Tundu Lissu kupitia kwenye majukwaa ya kisiasa kama ni za kwake au anatumwa na chama chake na ikithibitika Msajili wa Vyama vya Siasa achukue hatua kwa mujibu wa sheria kutokana kuwa kauli hizo zina lengo la kuligawa taifa letu," alieleza Khatib.

Vyama vilivyotoa tamko hilo ni ADA TADEA, CCK, NLD, Demokrasia Makini, NCCR-MAGEUZI, TLP, UPDP, SAU, UMD, NRA na Chama cha DP.

Ehee hiki kitakuwa kigingi cha kingine cha Lissu kama atapita kule ndani ya chama chake, yaani aelewe kwamba ataingia kwenye mapambano bila msaada wowote wa kuungwa mkono kutoka kambi ya wapinzani wenzao!

### KAULI KALIKALI

Ukitaka kujua kichwa cha mwanasiasa huyu kina shida, huku chama chake kikijiita chama cha demokrasia, sikia maneno aliyosema Lissu baada ya Mchungaji Msigwa ambaye tunajua alikuwa kwenye kambi yake, lakini alipotumia uhuru wake wa kikatiba na demokrasia yake kukihama chama hicho, Lissu alikaririwa akisema maneno haya:

"Kwa kujiunga na maadui wangu wa kisiasa sasa naye ni hasimu wangu... Nitakutana naye kama hasimu wangu wa kisiasa."

Hii ina maana gani? Lissu kwake siasa ni uadui na uhasama kama mnapishana itikadi, mitazamo, matakwa na vyama hata kama mlikuwa marafiki namna gani. Hii si ni hatari?

Kwa hiyo kauli kama hizi, pamoja na za kumkejeli Rais Samia kutokana na Uzanzibari wake, kukejeli sera za Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na hata kukejeli baadhi ya hatua zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ni vigingi kwake kupata urais. Watanzania ni watu waungwana. Wangependa kuongozwa na kiongozi mwenye kauli laini.

### KISHINDO CHA SAMIA

Ukiacha chama chake kama kitampitisha kuwa mgombea wao na wapinzani wenzao wakabadilika na kumuunga mkono, Lissu bado atakutana na kikwazo kikubwa kuliko vyote vya hapo juu, na si kingine bali ni Chama Tawala, CCM!

Hapa ndiyo utakuwa ndiyo mwisho wa ndoto ya Lissu kuiongoza Chadema kushika dola ya nchi hii, kwani atakutana na maji marefu ya Dk. Samia iwapo Mwenyezi Mungu atawafikisha wote wawili hadi Oktoba mwakani.

Achilia mbali kauli za Lissu za kumsema vibaya Dk. Samia kwa sababu ya kutoka upande wa pili wa muungano, lakini hata rekodi alizoziweka Mhe. Rais kwa hii miaka mitatu na ushei aliyoongoza taifa hili ni fimbo tosha kwa Makamu Mwenyekiti huyo wa Chadema.

Hakuna eneo ambalo Dk. Samia hajaligusa na kulifanyia kazi kama inavyostahili, kuanzia kwenye demokrasia ya ndani ya chama chake na nje, kupanua uhuru wa vyombo vya habari, miradi ya kimkakati, diplomasia ya kimataifa, utalii kama ile Royal Tour, sekta ya madini hususani katika kudhibiti uuzaji wa holela wa madini nje ya nchi na ukusanyaji mzuri wa maduhuli, uboreshaji wa Bandari, uhuru wa vyombo vya habari na kadhalika.

Rais Samia pia amekuja na falsafa ya R4 zinazohusu maridhiano, kustahimiliana, kuleta mageuzi kwenye nchi na kufanya mabadiliko/mageuzi chanya ya nchi. Ni kupitia falsafa hiyo amevifungulia vyama vya siasa kikiwemo Chadema kufanya siasa za wazi na maandamano, na kurejesha mazungumzo ya vyama ili kujenga mwafaka wa kitaifa na maridhiano.

Hapo nimegusia haya maeneo bila ya kuyachambua kwa undani kipi kimefanyika kwa kuwa tumeshafanya hivyo mara kadhaa kwenye gazeti hilo na kubwa zaidi Watanzania walio wengi wanaelewa fika kila jambo zuri lililofanywa na Serikali hii ya awamu ya sita chini ya Dk. Samia.

Kazi kubwa iliyobaki kwa Lissu ni kuomba demokrasia wanayoiimba na kuililia kwenye majukwaa ya kisiasa ichuke mkondo wake ndani ya hiki chama chao wanachokiita cha 'demokrasia' lakini kikiwa hakiendani na jina hilo. Hili pia limeshajadiliwa sana katika gazeti hili.

Kama kupitishwa kugombea urais hapo mwakani basi iwe kwa njia za kidemokrasia na kama kushinda au kushindwa itimie kwa njia ya matakwa ya wengi na kwa maamuzi yao binafsi na si kushinikizwa kwa njia yoyote ile.

Sisi tulio nje ya ulingo wa siasa za Chadema tunategemea huu ndiyo wakati sasa wa chama hiki kuuthibitishia umma wa Watanzania kwamba ni kweli demokrasia inatamalaki chamani; na hizi habari za udikteta ama kukomoana hazina nafasi ni majungu tu ya wapinzani wao!

Yale mambo ya tukose wote kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa mwaka 2015 ambapo aliyetarajiwa kugombea urais wa Chadema, Dk. Wilbrod Slaa alitupwa nje dakika za majeruhi na badala yake nafasi akapewa mwanachama wa CCM, marehemu Edward Ngoyayi Lowassa, haya hatuyategemei mwakani kujirudia!

Haiwezekani chama kinachojiita Chama Kikuu cha upinzani kiwe kinategemea wanachama wa CCM kama turufu ya kushinda Uchaguzi Mkuu ili kishike dola! Mpeni nafasi Lissu aje akutane na hasira za wananchi!

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.*

# Vijana wakati wenu huu, timizeni wajibu

**Na Hamid Yassin**

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM), Mohammed Ali Kawaida, amewasihi viongozi wa umoja huo kuanzia ngazi ya mikoa na wilaya zote nchini, kujifunza namna ya kuishi kwenye misingi ya uongozi kwa vitendo huku wakizingatia katiba, kanuni na miongozo ya Chama Cha Mapinduzi.

Pia amewataka viongozi hao ambao walishiriki mafunzo ya chuo cha umoja huo, Ihemi mkoani Iringa, kuhamasisha ushiriki wa vijana kikamilifu katika uandikishaji kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura lililofungiliwa rasmi Julai 20, 2024 mkoani Kigoma.

Kawaida ameyasema hayo alipokua anahutubia viongozi na watendaji wa UVCCM katika ufungaji wa mafunzo ya viongozi na watendaji wa umoja huo mikoa na wilaya zote nchi nzima yaliyofanyika Ihemi mkoani Iringa kuanzia Julai 11 hadi 17, 2024.

"Niwasihi sana nendeni mkaishi katika misingi ya uongozi kwa kuzingatia katiba, kanuni na miongozo ya Chama chetu," alisema.

Akaongeza: "Nimefurahishwa sana na namna ambavyo mmekua wasikivu, mmeishi kwa ushirikiano, mmeishi kwa umoja na kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika kipindi chote cha mafunzo yenu. Mmedhihirisha kuwa ninyi ni viongozi wa kweli na mmekua katika misingi ya uongozi ndani ya CCM."

Aidha, aliwasisitiza kudumisha ushirikiano na viongozi wa umoja huo wa vijana wa CCM na viongozi wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu katika maeneo yao.

Kawaida alisema ni vyema viongozi hao wakafuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama na kutangaza kazi nzuri zinazofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika maeneo yao.

Akizungumzia Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Kawaida alisema viongozi lazima wawe mstari wa mbele katika kuhamasisha vijana waweze kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji baadaye mwaka huu na kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwani 2025.

Mafunzo hayo yalifungwa na Mwenyekiti Kawaida kule Ihemi mkoani Iringa ambapo awali yalifunguliwa na Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel John Nchimbi Julai 11, 2024.

Naam; baada ya tabaruku hiyo ya Mwenyekiti wa UVCCM, Komredi Kawaida hebu tuwazungumzie hawa vijana ambao siku hizi wamegoma kabisa kuitwa 'Taifa la kesho'!

Mimi binafsi sielewi hii kauli ya vijana kuitwa 'Taifa la kesho' ilitoka wapi! Nani alianzisha na kwa masilahi ya nani na yepi?

Kwani hata waasisi wa taifa hili akina hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na wenzake wakati wanapigania uhuru wa taifa hili kutoka kwa wakoloni, hawakuwa wazee, bali vijana wabichi kabisa!

Lakini sisi wazee tuliozaliwa baada ya uhuru tumeikuta hii kauli mbiu ya 'Vijana taifa la kesho' na tumeishi nayo hivyo hivyo hadi kizazi hiki cha sasa ambacho kimekuja kuikataa kabisa tena kwa vitendo!

Siyo kwamba tu siku hizi vijana wanahimizana kushiriki katika chaguzi mbalimbali za nchi, lakini ukweli ndiyo wamesheheni kwenye nafasi za uongozi wa taifa hili hivi sasa.

Na wengi wao wameonesha kumudu mikikimikiki ya kupigania maendeleo ya taifa hili. Ama kwa maneno mengine ni kwamba hawajawaangusha waliowaamini!

Lakini kama wahenga walivyonena kwamba, kwenye msafara wa mamba na kenge wamo, wapo vijana wachache wamekurupukia uongozi lakini wamewaangusha waliowaamini!

Nawapongeza vijana wanapohimizana kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika nchi yetu.

Nawapongeza kwa sababu kiukweli mwaka huu umefua dafu kulinganisha na miaka mingine kwa vijana kuhimizana kuwania nafasi za uongozi tangu uhuru wa taifa hili.

Binafsi nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na safu yake yote kwa kuwa chachu kubwa katika hatima hiyo ya kuona vijana wakifurika kuwania uongozi wa taifa hili adhimu hapa duniani.

Nasema, "kwa kuwa chachu kubwa" kwa sababu hakuna ubishi hata chembe kwamba Rais Dk. Samia amewafumbua watu na hasa vijana macho kuwania uongozi; Na hii ni zawadi ya Manani kwetu kwa mtu ambaye ni mzalendo kwa watu wake.

Kivipi? Ndiyo; kwa sababu siku zote kiongozi mwenye maono anabeba msalaba mkubwa kuhakikisha watu wake wananeemeka katika kipindi chake cha uongozi. Anajua shida na matatizo yao ni mzigo wake.

Kana kwamba hiyo haitoshi ni kiongozi huyohuyo ndiye anayeweka msingi mkubwa wa maendeleo ya wananchi wake tangu ya kijamii hadi ya kitaifa.

Msingi huo lazima uende sambamba pasipo kuchuja kwa wananchi hao ambao siku zote ndiyo walinzi wa taifa lao.

Pamoja wimbo ule wa kwamba vijana ni 'Taifa la kesho', haimaanishi huko nyuma hakukuwa na viongozi vijana, walikuwepo wengi miaka ya mwanzo ya uhuru lakini kadiri miaka ilivyosonga ndivyo nao walipungua kwa kasi na kubaki wazee wengi wakishika hatamu ya kuongoza taifa hili.

Nasema si jipya kwa sababu, Baba wa Taifa hayati Mwalimu Nyerere aliweka msingi huu tangu akipigania uhuru wa nchi hii kuanzia mwaka 1954 aliposhiriki kuanzisha Chama cha kupigania uhuru cha Tanganyika African National Union (TANU).

Mwalimu, akiwa kijana wakati huo, akawa muwazi kabisa mapambano hayo yanafanywa na wote bila kujali kabila zao, asili zao, dini zetu wala ukanda.

Wazee wote walimshangaa lakini kadri siku zilivyokuwa zikisonga mbele walianza kumkubali na hatima yake wakakubali yeye apewe uongozi wa Taifa hili mwaka 1961 akiwa kijana wa miaka 39 tu.

Mwalimu alionesha thamani ya usomi wake, ujana wake, taaluma yake na thamani ya wazazi wake achilia mbali jamii na taifa la Tanganyika wakati huo hadi ilipoungana na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania.

Huu ndio ulikuwa ujana wa thamani na wa kheri kubwa kwa taifa hili na baadaye Afrika nzima kutokana na msimamo wake wa kuhakikisha watu wanakuwa huru ndani ya nchi yao na viongozi si wa nchi hizo tu bali pia Afrika nzima.

Mwalimu Nyerere alishirikiana na vijana wenzake wa Afrika wa wakati huo kama kina Nkwame Nkurumah, Anwar Sadat, Ahmed Sekou Toure, Patrice Lumumba, Abubakar Tafawa Balewa na wengine wengi kulikomboa Bara hili kutoka kwenye makucha ya wakoloni.

Mwalimu huyohuyo akaifanya nchi yake ya Tanzania kuwa kitovu cha uhuru wa Bara la Afrika pale alipowakaribisha hapa nchini wapambanaji kama vile akina Samora Machel, Robert Mugabe na wengineo wengi kwa ajili ya kujipanga na mapambano ya kuzikomboa nchi zao.

Kilichomfanya Mwalimu kujitosa katika hili ni kile alichokisema ambacho kinaishi hadi leo hii. Naomba nimnukuu; "Tanzania haitakuwa huru kama jirani zake watakuwa bado wakitawaliwa".

Tunaliona hili leo likifanywa na rais wetu, Dk. Samia pale anapoufufua na kuuimarisha ushirikiano wa kimataifa wa Tanzania na mataifa mengine ndani na nje ya Bara hili la Afrika.

*Inaendelea uk. 18*





# Tusidharau yanayotokea kwa jirani

**Na Dk Felician Kilahama**

Maandiko Matakatifu yanatutahadharisha kwamba: Kwa maana hakuna neno lililositirika, ila kusudi lije kudhihirika; wala hakuna lililofichwa, ila kusudi lije kutokea wazi. Mtu akiwa na masikio ya kusikilia, na asikie. Akawaambia, Angalieni msikialo; kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa. Kwa maana mwenye kitu atapewa, naye asiye na kitu, hata kile alichonacho atanyang anywa. (Marko 4: 22-25).

Kwanza, nikiri kuwa mimi sina utaalamu wa masuala ya thiolojia au ya kiroho ila kwa ufahamu wangu mdogo, hilo ni 'Neno la Injili kwa mtazamo wa Kiroho; ingawa walioambiwa zaidi ya miaka 2000 iliyopita ni binadamu kama sisi isipokuwa tofauti yetu na wao, sisi tunajali zaidi mifumo ya kidunia kuliko ya kiroho kutokana na ulimwengu kengeufu unaoshabikia kipato na hata maovu!

Kwa mtazamo wa macho ya kibinadamu harakaharaka utasema: kumbe ukiwa huna kitu badala ya kuongezewa kwa hicho kidogo ulichonacho, badala yake utanyang anywa! Wataalamu wa masuala ya kiroho wanafahamu halihalisi kuhusu matarajio ya kuufikia uzima wa milele huko mbinguni.

Lakini kwa hapa duniani haitofautiani na mtazamo aliokuwa nao Baba wa Taifa, Rais wa Kwanza wa Tanzania Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Wakati fulani aliwahi kusema: Waepuke sana mapebari ni manyang'au maana watu hao hawana huruma kwa maskini; wanachukua kila kitu na kuwaacha katika dimbwi la umaskini.

Vilevile, hakuna tofauti tunaposema 'walionacho wataongezewa na wenye kidogo watanyang'anywa' kwa maana kwamba mapebari ni wenye ukwasi wa juu sana au matajiri kupindukia lakini bado hawana huruma na maskini.

Mfano, mataifa kadhaa Afrika tuna rasilimali asilia za kutosha ikiwemo ardhi toshelezi; kutokana na kuwa duni kiteknolojia na mifumo husika ya kielekitroniki katika ulimwengu wa kidijitali; tunajikuta tunakaliwa na mabeberu na/au ukoloni mamboleo kiasi cha wao kuendelea kutajirika zaidi wakati huohuo wakijigamba kutafuta maisha mengine kwenye sayari zilizojuu angani!

Kilichotokea kwa jirani zetu hivi karibuni hadi moto ukawashwa nchi nzima na kusababisha vurugu za kila aina; kimejikita zaidi kwenye taswira ya Maandiko Matakatifu kama utangulizi halisi wa makala haya ulivyobainisha.

Huko wamebainisha kilichotakiwa kufanywa na Serikali waliyoiweka madarakani kwamba kinalenga kuwanyang anya hata hicho kidogo walichonacho kwa maslahi ya wachache; ndiyo maana wakaijia juu Serikali waliyoiweka. Nasema hayo ni madai ya wale vijana wanaojiita Gen Z ingawa sina uhakika wa madai yao walipoponga Muswada wa Sheria ya Fedha. Kwani sasa ni kama madai yao kisiasa zaidi kuliko maslahi ya wananchi!

Hata hivyo, kwa bahati mbaya, haikuwa rahisi kwa viongozi kusoma alama za nyakati, imewagharimu kiasi cha kujikuta katika hali isemwayo: muungwana ni vitendo na majuto ni mjukuu.

Vilevile, tumeonywa kupitia Maandiko Matakatifu kwamba, hakuna neno lililositirika, ila kusudi lije kudhihirika baadaye; wala hakuna lililofichwa, ila kusudi lije kutokea waziwazi na mtu akiwa na masikio ya kusikia, na asikie.

Kadhalika, tunatahadharishwa kwamba, kipimo kilekile tupimacho ndicho pia tutakachopimiwa, hata kuzidishiwa.' Hali kama hiyo maanake nini?

Haitofautiani pia tunavyoonywa kwamba katika kuishi kwetu hapa duniani tupendane kama Mungu wetu anavyotupenda na kututakia maisha mema.

Mpende jirani yako kama nafsi yako. Je, tunafanya hivyo? Kipimo tumpimiacho jirani yetu ndicho pia tutakachopimiwa? Kama wale Gen Z kuna mtu nyuma yao ana maslahi tofauti, labda ya kuwaondoa madarakani waliopo basi ajue kipimo hicho hicho linaweza kumpima pia!

Katiba yao ilibainishwa kuboreshwa kwa maslahi mapana ya taifa na watu wake; ikawa inasifiwa na wengi kuwa italeta mabadiliko makubwa kwenye mifumo ya kiutawala hata demokrasia na haki za binadamu.

Katiba nzuri inaweza ikawepo (ingawa uzuri ni majumuisho yenye mchanganyiko wa hisia na matakwa tofautitofauti); Sheria husika pamoja na kanuni zake, taratibu na miongozo husika vikawepo; lakini kukatokea sintofahamu kubwa kwenye tafsiri na mitazamo hasi hadi kupelekea kusababisha migawanyiko hususani tunapokuwa na mifumo ya utawala wenye mjumuiko wa vyama vingi vya siasa.

Wanasiasa wanapokuwa wakinadi sera zao na mitazamo kimaendeleo, kijamii na kiutamaduni, haitofautiani na halihalisi ilivyokuwa kwa nyoka mwerevu alivyomwendea Hawa/Eva akiwa peke yake katika Bustani ya Edeni (maandiko hayajatwambia Adam alikuwa wapi).

Lakini huyo nyoka kwa maneno matamu yenywe kumlaghai yakamwingiza huyo mwanamke wa kwanza katika uso wa dunia, kwenye matamanio ya kula alichokatazwa asile.

Hivyo Hawa/Eva akajikuta amekiuka agizo walilopewa na Mungu kutokula matunda ya mti uliopandwa katikati ya Bustani ya Edeni (Kitabu cha Mwanzo 3: 1-6) ikawa ni chimbuko kwa changamoto tunazokumbana nazo katika maisha duniani.

Nyakati za uchaguzi Watanzania huyatarajia mengi; ahadi nzuri zinazovutia pamoja na mipango/malengo kabambe kwa maendeleo ya watu.

Nia ni wapigakura wavutiwe na kuchagua watu watakaowavutia zaidi. Kimtazamo, kuvutiwa ni jambo moja na uhalisia wa mambo baadaye ni jambo jingine.

Nilichojifunza kutokana na kile kilichojitokeza kwa wenzetu ni kwamba katiba itakuwepo, sheria, kanuni kadhalika lakini wananchi wakaona vyombo hivyo haviwafai. Hasa wanapoona badala ya vyombo vya kisheria kuwepo kwa maslahi ya wengi, vinatumika kinyume na matarajio yao.

Kadhalika, wananchi wanapokuwa na uelewa/ufahamu toshelezi kutokana na mambo fulanifula kwenye 'mifumo' ya kiutawala na kadhalika; wakaanza kuhoji kwa nini hiki au kile; hapo mwenye masikio asikie yanayohojiwa pia kuchukua hatua stahiki mapema.

*Inaendelea uk. 18*





## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Hatua hii ya Bodi ya Mikopo kunoa wahitimu ya kupongezwa



Ukosefu wa ajira ni moja ya tatizo linaloikabili nchi yetu na kimsingi si Tanzania pekee bali na nchi nyingi duniani. Kutokana na tatizo hili, hatua madhubuti na stahiki zimekuwa zikichukuliwa na wadau wote muhimu yaani serikali, sekta binafsi, jamii na vijana wenyewe ili kuhakikisha kuwa fursa za kazi na ajira zinaongezeka ili kupunguza tatizo la ajira kwa kiasi kikubwa.

Uwepo wa idadi kubwa ya vijana mtaani huku kukiwa na fursa chache za ajira si jambo lenye afya. Ninajua serikali haijalala, inaendelea kuumiza kichwa katika kutatua tatizo hili na hata ule mpango wa Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) ni sehemu ya kupambana na changamoto ya ajira nchini.

Na wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Ridhiwani Kikwete kuhakikisha vijana wanapata kazi.

Rais alisema: "Kazi yako kubwa kwenye ile wizara ni uratibu wa kuhakikisha vijana wanapata ajira zao. Kunakuwa na uzalishaji wa kazi katika sekta nyingine, kilimo, madini, uvuvi kote kuna ajira kwa vijana. Nataka ukawe mratibu na ukahakikishe kila sekta inatoa ajira kwa Vijana na tukikuuliza Ridhiwani mpaka kufikia Desemba mwaka huu kama tupo Januari mwakani, tumetengeneza ajira ngapi uniambie kwenye finger tips kisekta, kilimo wapo hivi, ndio kazi yako. Kazi yako sio wewe kutengeneza ajira kwa vijana, kazi yako ni kuhakikisha sekta zinatengeneza ajira kwa vijana nawe unaratibu kazi lakini na haki zao."

Kimsingi, mafanikio katika sekta ya elimu nchini kuanzia elimu ya msingi, sekondari, vyuo na vyuon vikuu yamechangia ongezeko kubwa la wahitimu. Kumekuwa na uboreshaji mkubwa wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia huku serikali ikibeba mzingo wa kutoa ruzuku ya elimumsingi bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita ili kutoa fursa sawa kwa watoto na vijana wa Kitanzania kupata elimu bila vikwazo.

Na pale wanafunzi hao wanapofanya vyema katika mithani ya kidato cha sita na hatimaye kuendelea na masomo ya shahada katika vyuo vikuu, serikali imekuwa ikitoa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Haya yote yanafanyika kwa nia njema kabisa kuhakikisha vijana wa Tanzania wanakuwa na maarifa, ujuzi na stadi stahiki za kuwawezesha kujitegemea.

**Kazi yako kubwa kwenye ile wizara ni uratibu wa kuhakikisha vijana wanapata ajira zao. Kunakuwa na uzalishaji wa kazi katika sekta nyingine, kilimo, madini, uvuvi kote kuna ajira kwa vijana.**

Moja ya changamoto katika mfumo wetu wa elimu kabla ya maboresho ya mitaala yaliyofanyika ilikuwa ni ukosefu wa ujuzi wa kuwezesha vijana kuajiriwa au kujiajiri wenyewe baada ya elimu zao na wengine hata baada ya kozi.

Ni wazi wahitimu wa hatua mbalimbali wamekuwa wakiandaliwa kuajiriwa bila kuwa na stadi na ujuzi wa kujiajiri, hali hii ikapelekea Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuchukua hatua za kuziba udhaifu huu kwa kufanya maboresho ya mitaala ambapo sasa mafunzo ya amali yanapewa msukumo mkubwa ili kuwajengea uwezo wanafunzi kuwa na ujuzi wa kuwasaidia kujitegemea bila kutegemea ajira rasmi.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ni taasisi yenye dhamana ya kuchochea maendeleo ya elimu nchini kwa kutoa mikopo lakini pia kuwasaidia wanufaika wake wa mikopo kuwa na ujuzi stahiki ambao utakuwa nyenzo muhimu ya kuajiriwa na kujiajiri na hatimaye kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo waliyokopeshwa.

Ni katika muktadha wa kuwajengea uwezo wahitimu ili kuajiriwa kirahisi au kujiajiri, Bodi imeandaa mafunzo rasmi ya kuwasaidia wahitimu ili wawe na ujuzi ambao ni mtaji muhimu katika maisha yao, hasa baada ya kuhitimu masomo yao.

Bodi kwa kushirikiana na taasisi ya Adanian Labs wameandaa mafunzo kwa wanafunzi wa mwaka wa mwisho na wahitimu katika michepuo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehema) na sayansi ya kompyuta ili kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa na hivyo kuwa na vipato ambavyo pamoja na kuendesha maisha yao, watachangia maendeleo ya uchumi wa nchi lakini pia watakuwa na uwezo wa kurejesha fedha walizokopeshwa vyuoni.

Hivyo basi, Bodi, mbali ya kutoa mikopo na kuwadai wanufaika wake, sasa imeamua kujiongeza na kufanya jitihada za kuwatafutia fursa wanufaika wake ili wawe na uwezo wa kurejesha fedha na hatimaye wengine waweze kusoma kupitia marejesho ya fedha zao. Hii ni hatua murua na ya kupongeza sana.

Mafunzo haya muhimu yenye lengo la kuwajengea uwezo wanafunzi wa mwaka wa mwisho na wahitimu wa fani za Tehama na kompyuta ambao ni wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu yatasaidia sana kuwaongezea umahiri, stadi na ujuzi ambao ni muhimu sana katika kujitegemea kiuchumi badala ya kubaki nyumbani wakisubiri ajira rasmi serikalini au katika sekta binafsi.

Mafunzo haya yatatolewa bure kwa njia ya mtandao kwa kipindi cha miezi minne kuanzia Agosti 5, 2024. Kwa kuwa mafunzo haya yataendeshwa kwa njia ya mtandao, kila mwombaji anapaswa kuwa na kompyuta na intaneti ili kuweza kujifunza kikamilifu na kupata ujuzi na stadi muhimu.

Kwa ushindani uliopo sasa katika soko la ajira, mhitimu mwenye ujuzi wa kutosha anajiweka katika nafasi nzuri ya kuajiriwa na kujiajiri na ndiyo maana taasisi mbalimbali zinashauriwa kutoa fursa kwa wahitimu kujitolea katika taasisi zao ili kuwaongezea ujuzi wanafunzi na wahitimu kwani ujuzi huo ni muhimu katika kujitegemea kiuchumi.

Sanjari na hilo, uamuzi wa Bodi ya Mikopo kushirikisha wadau wengine kuwajengea uwezo wanafunzi na wahitimu ni wa kupongezwa kwani unasaidia moja kwa moja kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wa Tanzania kwa kuhakikisha wanapata ujuzi na stadi kuendana na mazingira, ushindani na soko la ajira.

Kwa wataalamu wa Tehama na kompyuta jitokezeni kwani fursa hii si ya kuichezea, ombeni kujiunga na mafunzo haya ili mjiongezee uwezo na ujuzi na hatimaye muwe na uwezo wa kujitegemea kiuchumi na kulipa fedha mlizosomeshwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o
KLINIKI YA FIKRA
Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

WEWORK CONSULT

# Dondoo za matumizi sahihi ya muda



Matumizi sahihi ya muda ni moja ya mambo muhimu kuyazingatia ili kufikia hatma unayoikusudia. Watu wengi wamekuwa wakiimba dhana hii bila mafanikio na kujikuta wakipoteza muda mwingi kwa vitu visivyo na matunda.

Tunapoongelea matumizi sahihi ya muda ni kuhakikisha muda wako unatumika kwenye vitu ulivyopanga na vinavyokuletea matokeo.

Leo Kliniki ya Fikra inaangazia dondoo muhimu zitakazokusaidia kuutumia muda wako vizuri. Tafadhali Fuatana nami: -

**KUWA NA MPANGO WA MAMBO YAKO (PLAN)**

Watu wengi wanaishi na kufanya mambo yanayokuja tu. Ni muhimu kupanga siku zako na kuhakikisha kila muda upo kwenye mpangilio.

Ukiweza kupanga ni hatua kubwa kukufanya utumie muda wako vizuri. Andaa ratiba yako ya siku, wiki au mwezi na hata mwaka ukionesha mambo muhimu kwa wakati husika, utayafanya lini na kwa rasilimali zipi?

Hakikisha una orodha ya mambo yako ya kufanya kila siku (To do List), tumia kalenda mtandao (Kama vile google calendar), weka vitu vya kukumbusha kama vile Reminders, Alarm, nk. Dalili ya mtu kufanikiwa ni kuwa na mpango rasmi wa mambo yake.

**KUWA NA VIPAUMBELE (PRIORITIES)**

Baada ya kuwa na orodha ya mambo ya kufanya, ni muhimu kuweka vipaumbele ili kujua nini kinaanza na kipi kunafuata. Ni muhimu ukiamka tu, uwe unajua ninaanza na nini na kinachofuatia ni nini.

**ANZA MAPEMA (START EARLY)**

Hii ni siri itakayokupa hamasa ya kuutumia muda wako vizuri. Ili kulifanikisha hili; lala mapema, lala saa za kutosha zinazoshauriwa kitaalamu, na ndipo utafanikiwa kuamka mapema na kuanza ratiba zako mapema. Pia ili ufanikiwe vizuri kwenye majukumu yako, anza kwa sala (maombi), anza na mazoezi mepesi kisha anza na mambo rahisi ili kukupa hamasa.

**CHANGANUA KILA JUKUMU LAKO (BREAKDOWN EVERY TASK)**

Ukijipa jukumu la kufanya, lichanganue vizuri. Mfano, ukiweka lengo la mwaka ni kujenga nyumba, basi anza kuchanganua lengo hilo kwenye "tasks" ndogondogo kama vile, lini unatakiwa kununua kiwanja, mpaka lini utanunua matofali, unahitaji cement ngapi, nondo ngapi, mbao kiasi gani, gharama ya ufundi ipoje, bati, milango, madirisha, umeme, bomba, nk. Hapa utakuta ndani ya lengo moja kubwa, kuna kazi au malengo madogo mengi. Haya yatakupa kujua sasa uhalisia wa ugumu au wepesi wa jukumu kuu.

**GAWA MAJUKUMU (DELEGATE TASKS)**

Kama upo na watu, ni vizuri sana ukigawa majukumu. Usilazimishe kufanya kila kitu mwenyewe. Hii itakupa faida nyingi kama kukamilisha mambo kwa haraka, kurithisha uwezo, kuwapa nafasi wengine kukua, itakuongezea uzoefu wa usimamizi, nk.

**WEKA MALENGO JANJA (SMART GOALS)**

Malengo yako ili yatimie hakikisha ni malengo mahsusi (Specific), yanayopimika (Measurable), yanatekelezeka (Achievable), ni malengo halisia (Realistic) na pia yawe na muda maalum na ukomo (Time bound). Malengo yenye sifa hizi, hayatakupotezea muda kwenye kuyasimamia kutimia.

**USITOKE NJE YA MALENGO (AVOID DESTRUCTION)**

Ukishaweka malengo ni muhimu sana kuwa makini na mwangalifu ili usitoke nje ya malengo. Hii inaitwa "Focus" Usianze kuvutiwa au kutamani malengo ya watu. Mfano social media, maongezi, wageni wengi na marafiki, kupokea majukumu ya kusaidia na kutamani njia za watu.

**SEMA HAPANA KWENYE BAADHI YA MAMBO**

Ili ufanikiwe kutumia muda wako sawasawa lazima uwe na uwezo wa kusema hapana kwenye mambo ambayo hayapo kwenye ratiba zako na hususani yale ambayo hayana mchango chanya kwenye malengo yako.

**SHUGHULIKIA MSONGO WA MAWAZO (AVOID STRESS)**

Ili kutumia muda wako vizuri shughulikia mambo yanayoweza kukutia kwenye msongo wa mawazo au kama tayari upo kwenye hilo tatizo basi shughulikia kwa hekima. Msongo wa mawazo una tabia ya kumpotezea muda sana mhusika na kumwacha kwenye njiapanda kwa muda mrefu.

**EPUKA KUFANYA MENGI KWA WAKATI MMOJA (MULT-TUSKING)**

Pamoja na kuwa utafiti unaoonesha kuwa wanawake wanaweza kufanya mambo kadhaa kwa wakati mmoja, lakini ni vizuri sana ukafanya jambo moja kwa wakati mmoja. Hii itakujenga zaidi kuliko kuwa na mambo mengi kwa wakati mmoja.

**PUMZIKA**

Ukitaka kuwa na matumizi mazuri ya muda, pumziko. Pumzika katikati ya kazi ili kurudisha umakini (Time off – 5 minutes room), fanya mapumziko ya mwili na jiburudishe (Refreshments)

**FUATILIA MALENGO YAKO KUHAKIKISHA YANATIMIA KWA WAKATI NA RASILIMALI ZILIZOPANGWA**

Hii itakufanya usisubiri hadi mwisho wa kazi kugundua kuwa kazi zooote zimeharibika uanze upya. Fuatilia kwa nyuma kuhakikisha kila kitu kinaenda vyema na maeneo ya kurekebisha, fanya mapema.

**JITATHMINI (EVALUATION)**

Hili ni jambo muhimu sana kwenye kutunza muda wako kwa sababu bila kujifanyia tathmini za mara kwa mara, utajikuta unarudia makosa yaleyale mara kwa mara, jambo ambalo ni upotevu mkubwa wa muda.

Wework Consult - Your Partner in Growth

# Wagombea Urais TLS

*Inatoka uk. 11*

**NITANG'OA MAFISADI TLS**

Kwa upande wake, Boniface Mwabukuzi anasema anataka nafasi hiyo ili kuleta mageuzi ambayo kwa muda mrefu yameshindikana ikiwemo kupambana na mafisadi kwenye chama hicho na nje ya chama.

Anasema TLS kwa muda mrefu imeshindwa kutimiza wajibu wake wa kusaidia wanachama kutokana na watu wanaochaguliwa kuiogopa serikali, hali ambayo iliwafanya washindwe kusimamia misingi ya kuanzishwa kwa TLS.

"Uadilifu ni jambo la msingi sana kwenye nchi inayojali demokrasia kwa hiyo nitasimamia suala hilo kwa dhati kabisa ili kurejesha heshima ambayo imeanza kupotea kwa watu kufanya mambo yasiyofaa kwenye fani ya uwakili," anasema.

**TLS NI NINI**

TLS ni chama cha kitaaluma cha mawakili wa Tanzania Bara kilichoanzishwa chini ya Sheria ya TLS ya mwaka 1954 ambayo inataja majukumu na kazi zake kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

TLS ina jukumu la kuhakikisha kuwa mawakili wanafuata viwango vya juu vya maadili na taaluma katika kazi zao za kisheria pamoja na kuweka kanuni na taratibu za maadili na kuchukua hatua dhidi ya mawakili wanaovunja kanuni hizo.

Chama hiki kinawajibika kutoa mafunzo endelevu kwa mawakili ili kuhakikisha wanabaki na ujuzi na maarifa ya kisasa katika nyanja mbalimbali za sheria na mafunzo haya ni pamoja na semina, warsha, na kozi za muda mfupi.

TLS ni sauti ya mawakili mbele ya serikali, vyombo vya sheria, na taasisi nyingine za kitaifa na kimataifa. Chama hiki hushiriki katika mijadala na kutoa maoni juu ya masuala ya sheria na sera za kisheria na kinajihusisha katika shughuli za kukuza na kulinda haki za binadamu nchini Tanzania pamoja na kutoa msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za mawakili.

Kupitia mipango mbalimbali, TLS inatoa msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji, hususani wale wasio na uwezo wa kulipa gharama za mawakili na hiyo inajumuisha kutoa ushauri wa kisheria na uwakilishi mahakamani.

Chama kinafanya kazi kwa karibu na mahakama na serikali kuhakikisha kuwa mfumo wa sheria unafanya kazi kwa ufanisi na haki na pia inahusika na kuhamasisha raia kufuata sheria na kuheshimu haki za kila mmoja.

**MANUFAA YA TLS**

Kwa kushirikiana na vyombo vya sheria na serikali, TLS inachangia kuboresha mfumo wa sheria na kuhakikisha kuwa unafanya kazi kwa haki na ufanisi na Kazi za TLS katika kuhamasisha haki za binadamu husaidia katika kujenga jamii yenye haki zaidi, ambapo haki za kila mtu zinaheshimiwa na kulindwa.

Kwa kutoa msaada wa kisheria kwa wale wasio na uwezo, TLS inasaidia kupunguza ukosefu wa haki kutokana na ukosefu wa uwakilishi wa kisheria na kupitia mafunzo na kuendeleza taaluma, TLS inahakikisha kuwa mawakili wanabaki na viwango vya juu vya ujuzi na maarifa, ambayo ni muhimu kwa utoaji bora wa huduma za kisheria.

Kwa kuwakilisha mawakili na maslahi yao, TLS inasaidia katika kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi ya mawakili yanaboreshwa, na hivyo kuimarisha sekta ya sheria kwa ujumla.

# Vijana timizeni wajibu

*Inatoka uk.14*

Ni wazi bila ubishi kuwa Dk. Samia anafuata nyayo za Baba wa Taifa katika kuliwezesha hili na leo hii Tanzania imerejea katika upendo mkubwa uliopotea wa nchi hizo na nyingine nje ya Afrika.

Lakini kwa nini Dk. Samia anakuwa msitari wa mbele katika masuala haya ya maendeleo ya kijamii, uchumi na uhusiano na nchi hizo? Ndiyo; yote hiyo ni kwa sababu Rais wetu huyu anaijua historia ya Afrika na dunia nzima.

Ni kwa msingi huu basi ndipo ninapokuja kwa dhati kabisa kusema kuwa vijana wetu wanaokimbilia uongozi lazima tuwapime kama wanaijua historia ya nchi hii na Afrika bila kusahau ya dunia.

Wawe kama Mwalimu Nyerere ambaye aliutumia ujana wake vyema kiasi cha wazee wenyewe wakiwemo viongozi wa dini, kumkubali na kuwa naye bega kwa bega kuelekea uhuru wa Taifa hili na Afrika nzima.

Vijana wetu hawa wanatakiwa wajue kuwa Rais Dk. Samia hakuzuka tu kama uyoga hadi leo hii kuwa Rais kama baadhi ya watu wanavyodhani.

Dk. Samia amekuwa mstari wa mbele na makini kila alipokuwa akipewa nafasi ya kuongoza, iwe idara, Wizara za serikali yetu, Naibu Spika wa Bunge la Katiba na hata pale alipokuwa Makamu wa Rais, hakuwaangusha waliomwamini.

Kwa hiyo, vijana wanaowania uongozi wa nchi hii lazima waelewe historia ya nchi hii kama anavyoijua Dk. Samia. Cha msingi zaidi wajiepushe na ufedhuli, wizi, ufisadi, ukuadi, ukibaraka na hasa wa nchi za nje ambazo hazina lolote zaidi ya kutaka tupigane wenyewe kwa



wenyewe ili wao wafaidike na utajiri wetu.

Vijana wetu wakilijua hilo, nchi hii itakuwa pepo ya dunia ikiwa na raha zote ambazo mtu anaweza kuzifikiri katika uhai wake.

Bahari tuliyopewa na Mungu, maziwa, mito, milima, mabonde, misitu, ardhi pevu na yenye utajiri, madini ya aina zote huku mengine yakiwa Tanzania tu na si kwingineko kokote kule, ni zaidi ya zawadi na utajiri unaotakiwa kulindwa kwa kumtukuza sana Mungu.

Naam; tulipokubaliana naye, yaani Dk. Samia, basi Mwenyezi Mungu hakututupa na leo hii tuko kwenye amani ya kheri huku tukiwasubiri vijana wetu wapambane kupata viti vya uongozi wa Taifa hili kuanzia uchaguzi huu ujao wa Serikali za Mitaa Novemba mwaka huu.

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.*

# Yanayotokea kwa jirani

*Inatoka uk. 15*

Hatua ya kufanya maamuzi sahihi na mapema huashiria kuwepo kwa halitulivu na amani kwenye jamii. Haki ikitendeka amani inatawala, na madukuduku yanapungua sana.

Nikirejea kwenye maandiko matakatifu, tunaonywa kuwa tunayotaka tutendewe hivyohivyo tuwatendee wengine, tuwajali wengine kama tunavyojijali. Imeandikwa mpende jirani yako kama nafsi yako (Law 19:18; Lk.10:27).

Vilevile, tunafahamu kuwa misingi ya haki ikiharibika swali huwa 'mwenyehaki atafanya nini?' Katika ulimwengu wa kiroho ni kuwaombea rehema/neema zake Mungu ili Mungu Mwenyezi awasaidie wanaopelekea misingi ya haki kukengeuka ili watambue hali hiyo na kurekebisha kwa kumgeukia Mungu na kutubu katika roho na kweli na hapo wapate maarifa ya kimbingu na kuwatendea haki viumbe wa Mungu ambao ni wanadamu wenzao.

Katika dunia, inafika mahali akili za wengi zinakengeuka na kuanza kuhoji kwa kudai haki zao. Wanaweza kuwa na madai ya kweli au ya hovyo lakini busara ni kutowadharau kwani wasiposikilizwa majanga hutokea hivyo Mungu anakuwa kando, ibilisi anajitutumua.

Ukisikia watu wanapaza sauti wakisema sasa tumechoka na dhuluma hiyo ni ishara ya kiibilisi kupelekea jamii kuwa katika machafuko.

Taifa lenye amani tutakuwa tumejifunza kitu kutokana na kilichojiri kwa wenzetu.

Kumekuwepo na madai ya Katiba mpya kwa mitazamo kuwa iliyopo haiendani na mazingira ya sasa.

Kuwepo na katiba kwa mazingira tuliyomo ni jambo jema lakini je, wengi masuala ya kikatiba tunayafahamu? Nibudi kuwepo katiba na sheria ya kutuweka sawa, hata hivyo misingi yake ikikengeushwa itabaki kuwa majuto ni mjukuu .

Sera, katiba, sheria na kanuni ziwe shirikishi na jumuishi kwa wote. Kusiwepo na mianya inayoweza kupelekea kundi fulani likapewa huduma zaidi kuliko wengine kwa fedha zinatokana na jasho la wote (kodi/tozo).

Katiba itakayowekwa (sijui lini), wahusika tujitahidi kuweka chombo hicho muhimu kwa mustakabali wetu, kiwezeshe taifa kuendelea kuwa katika hali ya utulivu na amani kupitia misingi bora na haki kwa Watanzania wote.

Naiangalia katiba na sheria husika katika picha ya Safina inayoelea majini bila kuwepo madhara yoteyote; kutokana ilivyotengenezwa kwa kuzingatia hekima na maarifa ya kimbingu.

Hatimaye iliweza kubeba watu na vitu vingi kulingana na uwezo wake bila upande mmoja kulemewa kiasi cha kuhatarisha maisha ya viumbe upande mwingine. Mwenyezi Mungu awajalie wanaohusika na uwekaji/uwepo wa sera, katiba, sheria na kanuni, wawe na busara, hekima na maarifa ya kimbingu.

Kama alivyomjalia Mfalme Sulemani, akaweza kufanya yote kwa hekima na maarifa mengi hadi kuushangaza ulimwengu, iwe hivyo kwa Tanzania.

Mungu akiwa upande wetu hakuna kitakachoharibika ili mradi tumtambue maana 'Yeye anatutakia mafanikio mema. Tutambue uwepo wake, tumche na tumwabudu katika 'Roho na Kweli'; tuondokane na roho za ubinafsi, ubadhilifu na unafiki tukitenda haki kwa wanazania wote.

Nikirejea Maandiko Matakatifu imeandikwa Lakini hekima itokayo juu kwanza, ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki. Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani (Yak 3:17-18).

Vilevile, tunatahadharishwa kwamba Na kazi ya haki itakuwa amani; na mazao ya haki yatakuwa ni utulivu na matumaini daima. Na watu wangu watakaa katika makao ya amani; na katika maskini zilizosalama na katika mahali pakupumzikia penye utulivu (Isa 32:17-18).

Tanzania, tukizingatia haya pamoja na uhilisia wa Sera, Katiba na Sheria; hakika Mungu atakuwa upande wetu na taifa letu litasheheni 'Neema za Kimbingu': tukidumisha, upendo, amani na kuthaminiana sisi kwasisi bila kutegemea sana wengine.

Mungu hakutuumba tuwe tegemezi bali tuwe na nguvu, tufanye kazi kwa bidii na maarifa kwa maslahi ya familia zetu, taifa kwa ujumla. Fedha iwe ni matokeo ya juhudi zetu kupitia kazi na ubunifu wetu, tukizalisha mali, tukihudumiana kupitia baraka zake Mungu tunayemwabudu na kumtumikia.

Utajiri wa Tanzania uwe chachu kubwa kwa maendeleo endelevu kwa wananchi wote.

Nimalizie kwa kusema kwamba Rais wetu amakuja na falsafa ya R4, maridhiano, kustahimiliana, kuleta mageuzi/mabadiliko na ujenzi mpya wa nchi yetu.

Tukiziishi hizo R4 kila kitu naamini kitakwenda sawia.

# RSF wameua watu 65 katika mji wa El-Fasher



**KHARTOUM, Sudan**

TAKRIBAN watu 65, wengi wao wakiwa watoto, wameuawa tangu Jumamosi katika mashambulizi ya mabomu yaliyofanywa na wanamgambo wa kikosi cha Rapid Support Forces (RSF) katika mji wa Jimbo la Darfur wa El-Fasher, wanaharakati wamesema.

Mji huo wa Jimbo la Darfur Kaskazini, ndiyo mji mkubwa ambao haujadhibitiwa na kundi la RSF na wameuzingira tangu Mei, mwaka huu.

Vita kati ya RSF na Jeshi la Sudan, vimepamba moto tangu vilipozuka Aprili, mwaka jana.

The El-Fasher Resistance Committee Jumatatu walisema katika taarifa kwamba "Kwa kipindi cha siku tatu, RSF waliua zaidi ya watoto 43, wanawake 13 na wanaume tisa miongoni mwa wakazi wa El Fasher."

"Leo ni moja ya siku za mauaji mabaya mjini El-Fasher, dhidi ya raia, misikiti, hospitali, hasa hospitai ya Saudi," Gavana wa Jimbo la Darfur, Mini Minawi aliandika kwenye mtandao wa X.

Chanzo cha matibabu katika hospitali ya Saudi, ambayo ilishambuliwa vikali, awali kilisema shambulizi la mizinga liliua watu 22 siku ya Jumamosi.

Minawi aliongeza kuwa RSF walipokea siku mbili zilizopita mfumo wa makombora kutoka El-Geneina, Mji Mkuu wa Darfur Magharibi.

VOA.



## Kamanda wa mamluki la Urusi auawa Mali

**BAMAKO, Mali**

KAMANDA wa kundi la mamluki la Urusi, ameuawa nchini Mali kufuatia shambulio la wapiganaji wa waasi wakati wa dhoruba ya mchanga, kundi hilo lilisema.

Utawala wa kijeshi katika jimbo hilo la Afrika Magharibi, uligeukia kundi la Wagner mwaka 2021, kutafuta uungwaji mkono katika kupambana na vikosi vya jihadi na wanaotaka kujitenga.

Siku ya Jumatatu, kundi la Urusi - ambalo sasa limejigeuza kuwa kundi linaloitwa Africa Corps yaani Kikosi cha Afrika, lilisema limejiunga na Jeshi la Mali katika vita vikali dhidi ya waasi wanaotaka kujitenga na wanamgambo wa jihadi wiki iliyopita.

Hata hivyo, watu wanaotaka kujitenga, walifanya shambulizi kubwa na kuua takriban mamluki 20 hadi 50, vyanzo vya karibu na Africa Corps viliiambia BBC.

Vile vile, wanablogu kadhaa wa kijeshi wa Urusi, waliripoti kwamba takriban watu 20 waliuawa katika shambulio la kuvizia karibu na mji wa kaskazini-mashariki wa Tinzaouaten.

Katika taarifa rasmi iliyotumwa kwa telegram, kundi la mamluki la Urusi halikubainisha ni wanajeshi wangapi waliofariki dunia, lakini walithibitisha kupata hasara.

Hii ni pamoja na Kamanda, Sergei Shevchenko, ambaye aliuawa wakati wa makabiliano.

Hapo awali, mamluki hao waliwaangamiza Waislamu wengi na kuwafanya wengine kukimbia, ilisema taarifa hiyo. BBC.

## IMF yaidhinisha mkopo wa Dola bil. 3.4 kwa Ethiopia

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

ETHIOPIA yenye matatizo ya fedha, Jumatatu ilipunguza viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni kama sehemu ya mpango mpana wa mageuzi ya kiuchumi, huku Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF), likiidhinisha mkopo kwa taifa hilo ambalo linatafuta mabilioni ya Dola kujikwamua kiuchumi.

Thamani ya sarafu ya ndani, Birr, ilishuka kwa karibu asilimia 30.

"Mageuzi haya yanaleta ushindani unaotegemea soko la kiwango cha ubadilishaji wa fedha na kushughulikia mapungufu ya muda mrefu ndani ya uchumi wa Ethiopia," Benki ya Taifa ya Ethiopia (NBE), ilisema katika taarifa.

Nchi hiyo ya pili yenye idadi kubwa ya watu barani Afrika, ina matumaini ya kupata angalau Dola bilioni 10.5 kutoka kwa wakopeshaji wa nje ikiwemo IMF, lakini mazungumzo yamechukua muda mrefu na yamekuwa magumu.

Bodi ya IMF Jumatatu iliidhinisha mpango wa miaka minne wa Dola bilioni 3.4 kuunga mkono mageuzi hayo, huku Dola bilioni moja zikitolewa mara moja.

"Huu ni wakati wa kihistoria kwa Ethiopia, na mkopo huu ni ushahidi wa "dhamira kubwa ya nchi hiyo katika kuleta mageuzi", Mkurugenzi Mkuu wa IMF, Kristalina Georgieva, alisema katika taarifa. VOA.



## Watoto wawili wauawa, tisa wajeruhiwa shambulio la kisu

**LONDON, Uingereza**

WATOTO wawili wameuawa na tisa kujeruhiwa vibaya huku sita wakiwa mahututi katika shambulio la kisu kwenye warsha ya watoto kucheza densi.

Watu wazima wawili pia wako mahututi baada ya kudungwa visu walipokuwa wakijaribu kuwalinda watoto katika hafla iliyokuwa imepewa jina la Taylor Swift kwenye Mtaa wa Hart huko Southport, Polisi wa Merseyside walisema.

Mvulana mwenye umri wa miaka 17 kutoka Banks huko Lancashire, amekamatwa kwa tuhuma za mauaji na jaribio la kuua.

Polisi walisema sababu ya shambulio hilo haikuwa wazi, lakini haikuchukuliwa kama yenye kuhusishwa na ugaidi.

Shahidi mmoja alielezea tukio hilo kama la kutisha na akasema "hawajawahi kuona kitu kama hicho."

Mfalme na Waziri Mkuu, wameongoza kwa salamu za rambirambi kwa wale walioathiriwa.

Polisi wa Merseyside walitangaza kutokea kwa tukio kubwa baada ya kupokea simu za dharura saa 11.47 saa za eneo, wiki ya kwanza ya likizo za shule wakati wa majira ya joto kwa watoto wengi nchini Uingereza.

Magari ya kujihami, ya kubeba wagonjwa 13 na zima moto, yalikimbilia eneo la tukio ambapo tamasha la watoto wenye umri wa kati ya miaka sita na 10 lilikuwa likifanyika.

BBC.

## Waandamanaji watinga kambi ya jeshi

**YERUSALEM, Israel**

WAANDAMANAJI wa Israel wenye misimamo mikali ya mrengo wa kulia, wameingia kwenye kambi ya jeshi wakionyesha kuunga mkono wanajeshi wanaotuhumiwa kwa kumdhulumu mfungwa wa Kipalestina anayezuiliwa eneo hilo.

Umati mkubwa wa watu ulikusanyika nje ya kambi ya Sde Teiman baada ya polisi wa kijeshi wa Israel, kuwakamata wanajeshi wa akiba, ambao kwa sasa wanachunguzwa.

Kambi ya Sde Teiman karibu na Beersheba Kusini mwa Israel kwa miezi kadhaa, imekuwa ikiangaziwa kutokana na ripoti za unyanyasaji mkubwa dhidi ya wafungwa wa Gaza.

Siku ya Jumatatu, makumi ya waandamanaji, wakiwemo wabunge wa siasa kali za mrengo wa kulia kutoka muungano unaoongoza wa Israel, waliingia kwenye kambi hiyo na wengine wakijaribu kukwea ua huku wakiimba "hatutawaacha marafiki zetu, hakika si kwa ajili ya magaidi."

Baadhi ya wanajeshi katika kambi hiyo inasemekana walitumia maji ya pilipilidhidi ya wanajeshi waliofika kuwakamata wanajeshi wa akiba.

Waandamanaji pia walikusanyaka katika kambi ya kijeshi ya Beit Lid katikati mwa Israel ambapo wanajeshi wa akiba walipelekwa kuhojiwa.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alitoa taarifa akilaani vikali uvamizi huo wa kwenye kambi na kutoa wito wa kutuliza joto hilo"mara moja. Waziri wa Ulinzi, Yoav Gallant, alisema uchunguzi wa mienendo ya wanajeshi, lazima uruhusiwe kuendelea na kuongeza "hata wakati wa hasira, sheria inatumika kwa kila mtu."

Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari vya ndani, takriban wanajeshi tisa wa Israel katika kambi hiyo, wanatuhumiwa kwa kumdhulumu mfungwa wa Kipalestina, anayeshukiwa kuwa mpiganaji wa Hamas ambaye alitekwa Gaza.

Inasemekana amelazwa hospitalini baada ya kile ripoti za vyombo vya habari vya Israel kueleza kuwa ni unyanyasaji mkubwa wa kingono na majeraha kwenye sehemu yake ya haja kubwa na kusababisha kushindwa kutembea.

HABARI ZIMEANDALIWA NA **Hamid Yassin**

# ‘Wafia dansi’ wasaka udhamini



MRATIBU wa Tamasha la ‘Usiku wa Wafia Dansi’, Bernard James amewaomba wadhamini kujitokeza kwa wingi kudhamini tamasha hilo ili lifane zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Tamasha hilo lenye lengo kubwa la kukuza muziki wa dansi, kutoa ajira, kukuza sanaa, kuleta ubunifu na ushindani kwenye dansi, kuutangaza muziki wa dansi na kutoa burudani litafanyika jijini Dodoma Agosti 2.

Bernard amesema wadau wakijitokeza kudhamini tamasha hilo watapata fursa ya kutangazwa kwenye redio, televisheni, mitandao ya kijamii, kwenye mabango, kushiriki vipindi mubashara, kujitangaza siku ya tamasha pamoja na kuuza bidhaa, jina, kupata wateja wapya na kujenga taswira nzuri zaidi.

“Matangazo mengi unayaona kwenye mitandao kibao ya kijamii hasa Whats App, Instagram, Facebook, YouTube huku mengine yakipigwa redioni, pia siku ya tamasha litarushwa mubashara kwenye kituo kikubwa cha Star TV, sasa hapo huoni wadhamini watapata faida kubwa?” Amehoji Bernard.

Bernard amewaomba wafanyabiashara wakubwa, wadogo, wa kati na wajasiriamali kuitumia vyema fursa ya tamasha hilo kufanyika jijini Dodoma kujinadi.

“Watanufaika zaidi maana sikukuu ya wakulima ya Nane Nane kitaifa itafanyika mkoani Dodoma, sasa wanaweza tumia fura hiyo kutangaza na kuuza bidhaa, huduma, brandi zao na kueleza mafanikio na mipango yao kupitia tamasha hilo,” amesema mdau huyo wa muziki wa dansi.

Bernard amesema mpaka sasa wadhamini waliodhamini ni Star TV, Redio Free Afrika, Kiss FM, Cheza Kidansi, BJ Fashion, C FM, Royal Village Hotel Dodoma.

Tamasha la ‘Usiku wa Wafia Dansi’ liliasisiwa mwaka 2018 jijini Dar es Salaam kisha likafanyika mfululizo katika mikoa ya Morogoro, Mwanza, Arusha, Dar es Salaam na sasa Dodoma.

# Aslay awashangaa ‘wanaochimba’ masiha yake



NYOTA wa Bongo Fleva, Aslay amevunja ukimya kuhusu watu wanaoingia kwenye ukurasa wake wa Instagram na kuhoji kuhusu mtindo wake wa maisha na kudai yanamchukiza.

Hata hivyo, Aslay amesema hivi wala hajali wanavyomwongelea na kusisitiza kamwe hayatamrudisha nyuma kisanii na kumfanya kuwa mnyonge ingawa amekiri wakati mwingine inakera na anaamini wanaofanya hivyo ni wale waliokosa kazi na ndiyo maana wanafuatilia mambo ya watu.

“Huwa nakerwa na kushangazwa sana na hili jambo, sijui wanaofanya hivyo au wanadhani kukomenti vitu vya ajabu ajabu mara sijui koneksheni ndani ya peji yangu watanishushia heshima?” Amehoji Aslay na kuongeza.

“Hawanitii unyonge, ila ni kuonyesha wamekosa cha kufanya, wabadilike dunia inaenda kwa kasi,” alisema Aslay aliyeibuliwa na Kituo cha Mkubwa na Wanawe kabla ya kutamba na kundi la Yamoto Band akiwa sambamba na Mbosso, Beka Flavour na Bella.

Hivi karibuni msanii huyo anayetamba na ngoma kama ‘Hutegeki’, ‘Inauma’, ‘Pusha’, ‘Shuu!’, ‘Mhudumu’, ‘Mateka’, ‘Nashangaa’, ‘Usiitie Doa’ na nyinginezo amekuwa akijadiliwa na mashabiki mtandaoni kutokana na maisha yake na wengine wamekuwa wakiona kuna mambo anafanya sio mazuri, lakini mwenyewe amesema kwa sasa hajali wanachojadili na anaendelea na maisha yake.

# Miaka mitatu bila Waziri Ally

**Na Mwandishi Maalumu**

JULAI 23 mwaka 2021 wingu jeusi la huzuni lilitanda ghafla katika anga ya muziki nchini Tanzania kufuatia kifo cha ghafla cha mwanamuziki na kiongozi wa Bendi ya Njenje, Waziri Ally Seif ‘Kissinger’.

Waziri alikuwa mwanamuziki mwenye upeo na elimu kubwa ya muziki. Muungwana wa hali ya juu sana. Mwenye moyo wa huruma usiyomithilika.

Uwezo wake wa kupapasa kinanda, kupangilia muziki pamoja na kuimba haukuwa na mfano. Mwenyezimungu azidi kumwondolea adhabu ya kaburini kaka, akusamehe makosa yako na kukujaalia pepo yake Inshaalah.

Moja kati ya wapiga kinanda hodari sana kutokea Tanzania, elimu ya msingi na upigaji wa kinanda aliipata katika shule ya msingi iliyokuwa inamilikiwa na Kanisa katoliki maeneo ya Chumbageni Tanga mjini ikijulikana Kwa jina la St. Antony De Souza kwa sasa Changa Primary school.

Wazir Ally alijiunga na bendi ya JUWATA Jazz akiwa kijana mdogo kabisa kiasi wanamuziki waandamizi wa bendi hiyo walimkataa wakiamini hawezi kufanya kitu kwa umri wake

Lakini alifanya vitu vikubwa mno, ukitaka kuamini unyama wa Waziri Ally sikiliza vibao kama vile ‘Sogea karibu’, ‘Fatuma Maisha ni Vita’ na ‘Ete’.

Kulingana na wanafamilia Waziri alifariki baada ya kuugua ghafla na kuharakishwa katika hospitali ya Mwananyamala mjini Dar es salaam, lakini kwa bahati mbaya ilishindikana kuokoa maisha yake. Yote hiyo ilitokana na mapenzi yake Mwenyezi Mungu.

Waziri alikuwa kiongozi wa bendi ya Kilimanjaro kwa miaka mingi akishirikiana na wanamuziki wengine mashuhuri kama vile marehemu Mabruk “Babu Njenje” Hamisi, Mohamed Mrisho, Nyota Waziri, Keppy, John Kitime na wengineo

Waziri alianza kupiga muziki akiwa mdogo sana na bendi za muziki wa taarab mjini Tanga kama vile Lucky Star na Black Star. Uhodari wake wa kupiga kinanda ulimpa umaarufu hadi kuajiriwa na bendi za muziki wa dansi kama ya JUWATA Jazz ya mjini Dar es salaam.

Baadaye Waziri alijiunga na bendi ya vijana wenzake kutoka mjini Tanga, Kilimanjaro Band katika miaka ya 80 na kuanzia hapo hakutoka katika bendi hiyo hadi alipochukua uongozi wake katika miaka 90 baada ya kifo cha aliyekuwa kiongozi wa bendi hiyo Hemed Chuky.

Waziri aliiongoza bendi ya Kilimanjaro katika mikataba mingi ya kimataifa iliyowawezesha kupiga muziki katika nchi za Japan, Uingereza na nchi Falme za Kiarabu.

Baada ya kutoa albamu ya ‘Njenje’, ambayo ilifanya bendi hiyo kujulikana kwa jina la Njenje Kilimanjaro Band, ilitoa albamu nyingine kadha zikiwa na nyimbo ziligonga chati kama vile ‘Boko’, ‘Kinyaunyau’, ‘Kachiri’, ‘Tupendane’, ‘Ndembele’, na ‘Ndugu Zangu’.



# Nandy ashukuru miaka miwili ya ndoa



MWIMBAJI nyota wa muziki wa kizazi kipya, Faustina Charles Mfinanga almaarufu kama ‘Nandy’ amemshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutimiza miaka miwili ya ndoa na mumewe, Nichoaus Lyimo ‘Billnass’

“Mume wangu miaka miwili ya ndoa yetu imekuwa fundisho kubwa kwangu kujua upendo ni kitu muhimu sana, uwepo wako umerahisisha maisha yangu na ya kipenzi chako Naya (mtoto wao), jua tu tunakupenda sana. Ninachokuomba najua wanaume mmeumbiwa kupepesa macho japo sio mwanaume wangu wewe, popote uendapo, chochote ufanyacho jua una watu wanakupenda na kukuhitaji sana,” amesihi Nandy na kuongeza.

“Jitahidi kuyashinda majaribu, siku hizi ni rahisi sababu kila kitu kishapitwa na wakati na wakati wenyewe ndiyo sasa kuonyesha mfano na kuwa mifano bora kwa watu wenye mapenzi ya kweli, onyesha kuwa vijana wakiamua inawezekana. Mungu wangu atulinde nitimize ahadi ya watoto wako 10! Nakupenda.”

# Korosho Queens ni watoto wadogo wanaosulubu wakongwe




**Na Valensi Mbaga**

MPIRA wa wavu ni miongoni mwa michezo bora sana kwa kizazi cha sasa na kwa Tanzania, mchezo huu sasa unakuwa kwa kasi sana huku ikiibua vipaji vikubwa kutoka katika kona mbalimbali za nchi.

Jitihada kubwa za kukuza mchezo huu zinazofanywa na Shirikisho la mpira wa wavu Tanzania (TVF) imefanikisha kupeleka mchezo huu katika viwango vya juu zaidi.

Zipo timu mbalimbali ambazo zinachipukia na sasa zina viwango bora sana, lakini leo katika makala haya tutawaongelea vijana wadogo ambao wamefanya makubwa sana tangu mwaka 2012 mpaka sasa.



Hawa wamejitengenezea mashabiki wengi na nguvu kubwa sana ya kiuchezaji huku wakiziongoza timu zao kupata ushindi dhidi ya timu bora hapa Tanzania na hata nje ya mipaka ya nchi. Timu hizo ni pamoja na:

**Korosho Queens**

Zamani ilikua ikijulikana kama Mkalapa jina ambalo ni chimbuko la kijiji ambapo timu hii ilianza chini ya mwalimu Gabriel Joshua na baada ya usajili rasmi wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) Machi 15, 2023, ilibadili jina na sasa inajulikana kwa jina la Korosho Queens Volleyball Club.

Wakichukua jina la zao maarufu la biashara na chakula kwa wakazi wa mikoa ya kusini mwa Tanzania (Lindi, Mtwara na Ruvuma) ambapo wachezaji wengi wanaounda kikosi cha Korosho Queens wanapatikana katika mikoa hiyo.

Makao makuu ya Korosho Queens yanapatikana Mtwara mjini na ofisi ndogo ipo katika mji wa Masasi uwanja wa Bomani unaotumiwa na klabu ya Korosho Queens kama uwanja wake wa mazoezi.

Korosho Queens ni moja kati ya vilabu bora sana vya mpira wa wavu kwa upande wa wanawake na ni silaha kubwa katika kutangaza mpira wa wavu wa Tanzania kimataifa zaidi.

Korosho Queens Volleyball Club walifanikiwa kupata ubingwa wa Afrika Mashariki katika mashindano ya shule za Afrika Mashariki FEASSA 2022 na 2023 mfululizo ambapo wachezaji wote waliounda timu ya ubingwa huo ni wachezaji chipukizi kutoka katika akademi ya Korosho Queens.

Wachezaji wa timu hii ni vijana wadogo wanaosoma shule za msingi na sekondari ambao pia huziwakilisha shule zao katika mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA.

Matunda haya ni faida ya uwekezaji bora uliofanyika na Bodi ya Korosho huku wakiendelea kumuamini mwalimu Gabriel Joshua kukinoa kikosi hiki, mtaji ambao umelipa sana kwani kwa sasa Korosho Queens ni moja ya timu tishio katika michuano mbalimbali inayoshiriki.

Kocha Gabriel Joshua alithibitisha kukinoa kikosi hiki akianzia ngazi ya vijana wadogo ambao wanapata mazoezi sahihi kwa ajili ya mchezo wa wavu na baadaye kuja kuwa mabingwa na sio wachezaji tu.

Ligi ya Taifa ya mpira wa wavu (TVNL) imetamatika katika raundi ya kwanza na Korosho Queens wakiwa kinara huku ikizichapa timu imara na zenye ubora kama Tanzania Prison, Bandari, Jeshi Stars na JKT. Katika mchezo wa mwisho Korosho Queens iliwalaza Mafinga Parish na viatu kwa kuwapiga seti tatu kwa bila (3 - 0) na kuwa timu kinara katika mashambulizi yaliyofanikiwa zaidi (Spiking)

Korosho Queens imeundwa na vijana wadogo ambao wengi wao wako katika usawa wa elimu ya msingi pamoja na sekondari.

Kikosi hiki kina ubora katika kila kona lakini wapo wachezaji wake kama Wamada Salum ambae ni mshambuliaji (Spiker) na amefanikiwa zaidi kuziadhibu timu pinzani pale wanapomuachia upenyo mdogo tu.

Pia kuna Latifa Seif ambae ndiye aliyeibuka mchezaji bora katika michuano ya Kombe la Taifa mwaka 2023 na kwa sasa ana ubora mkubwa zaidi na kuwa moja ya silaha hatari kwa kocha Gabriel Joshua katika kujenga mashambulizi.

Lakini pia wapo nyota wao chipukizi kama Vannesa John, Reka Ally, Mwasiti Ismail, Wamada Salum, Gaudencia Paulo na Asnat Abbas ambao kwa pamoja wanatengeneza kikosi cha kwanza bora ambacho kimefanikiwa kutwaa mataji mengi zaidi.

Kikubwa cha kushangaza katika timu hii ya Korosho Queens ni umri ambao vijana hawa wanao. Wastani wa umri wa timu hii ni miaka 15 tu, lakini maajabu wanayoyafanya uwanjani huwezi kuyategemea na wamethibitisha hayo kwa kucheza na timu kubwa kama Tanzania Prison yenye wachezaji wengi wazoefu na wenye wastani wa umri kati ya miaka 21 hadi 30 na kupata ushindi.



# Nyota wa kimataifa wa kuwatazama Olimpiki 2024

**PARIS, Ufaransa**

TAKRIBANI wanamichezo 10,500 kutoka kote ulimwenguni watashiriki katika michezo 32 kwenye michuano ya Olimpiki hapa Paris msimu huu wa joto.

Hapa tunakuletea nyota wakubwa na mafanikio yao katika mashindano haya ya kimataifa.

**Leon Marchand (Ufaransa) - Kuogelea**

Bingwa huyo mara tano wa dunia anatazamiwa kushinda medali nyingi za dhahabu kwenye mchezo wa kuogelea.

Marchand mwenye umri wa miaka 22, ni mwanafunzi wa sayansi ya kompyuta katika chuo kikuu nchini Marekani, anajuulikana kwa kuvunja rekodi.

**Simone Biles (US) - Sarakasi**

Miaka mitatu iliyopita watu wengi walidhani, hawatamuona tena Biles baada ya michezo ya Olimpiki.

Biles alijiondoa katika mashindano kadhaa katika michezo ya Tokyo. Alichukua mapumziko kabla ya kurudi kwenye mashindano Juni 2023.

Biles tangu wakati huo amepata medali tano za ubingwa wa dunia, zikiwemo dhahabu nne. "Nahisi kujiamini sana kiakili na kimwili," alisema mwaka huu.

**Novak Djokovic (Serbia) - Tenisi**

Dhahabu ya Olimpiki ndiyo tuzo kubwa ambayo haipo kwenye mkusanyiko wa tuzo zake. Lengo lake mwaka huu katika mashindano ya Olimpiki ya Paris 2024, ni kupata medali hiyo.

Mwaka huu kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, haukuwa mwaka bora, hajashinda taji lolote na hayuko tena kileleni mwa viwango vya ulimwengu.

Jeraha lilikatiza michuano yake ya French Open kabla ya robo fainali. Ingawa alifika fainali ya Wimbledon mwezi huu kwa kufungwa goti, lakini alizidiwa kwa kiasi kikubwa na Carlos Alcaraz.

Hata hivyo, ikiwa yuko fiti, anaweza kupata hata shaba kama alioshinda Beijing 2008.

**Ledecky (US) - Kuogelea**

Je, kuna mtu yeyote anaweza kumzuia bingwa huyo wa mara saba wa Olimpiki?

Akiwa yuko tayari kushiriki mara ya nne, Ledecky mwenye umri wa miaka 27, anatajwa kuwa mwogeleaji wa kike aliyefanikiwa sana katika Olimpiki.

Ana nafasi ya kuweka rekodi kwani anatarajiwa kushindana katika matukio manne – mita 400, mita 800, mita 1500 na mita 4x200.

Ana medali 10 tayari, Ledecky anaweza kuvunja rekodi ya Jenny Thompson mwenye medali 12 ikiwa atashinda zaidi.

**Noah Lyles (US) - Mkimbiaji**

Mkimbiaji wa Marekani amejiwekea malengo makubwa.

Analenga kuwa mwanariadha wa kwanza kushinda medali nne za dhahabu kwenye mbio hizo za Olimpiki, akilenga kushinda katika mbio za mita 100, 200 na 4x100 na 4x400 za kupokezana vijiti.

Alishinda dhahabu katika mashindano matatu ya kwanza kati ya mashindano hayo kwenye mashindano ya dunia mwaka jana.

Ikiwa hilo halitoshi, ana malengo ya kushinda rekodi za dunia za mita 100 na 200 za gwiji wa Jamaica Usain Bolt.

Tangu achukue medali ya shaba ya mita 200 huko Tokyo 2020, Lyles ametawala mbio kwenye jukwaa la kimataifa na anaonyesha kipaji na ushujaa ambao unaweza kujaza pengo la Bolt tangu astaafu 2017.




**Faith Kipyegon (Kenya) - Mkimbiaji**

Bingwa wa Olimpiki mara mbili wa mbio za mita 1500 na anashikilia rekodi ya dunia kwa umbali huo.

Mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 30 anawinda medali mbili za dhahabu mjini Paris atakapo rudia mbio za mita 1500 na 5,000, kama ilivyokuwa katika mashindano ya dunia ya mwaka jana.

Kipyegon alianza maisha yake ya riadha akiwa na umri wa miaka 16 na alishinda taji lake la kwanza la kimataifa akikimbia bila viatu katika mashindano ya World Junior Cross Country Championships mwaka 2011.

**Neeraj Chopra (India) – Mrusha mikuki**

Ni maarufu sana nchini India na ana wafuasi milioni tisa kwenye Instagram.

Mwanamichezo wa kwanza wa India kushinda medali ya dhahabu ya Olimpiki, Chopra ana lengo la kutetea taji lake katika kurusha mkuki mjini Paris.

Mafanikio yake ya kushangaza huko Tokyo, ambapo pia alikuwa mwanamichezo wa kwanza wa Asia kushinda dhahabu ya Olimpiki ya mkuki.

Miongoni mwa wanaoweza kumpa changamoto ni Arshad Nadeem kutoka Pakistani - taifa hilo ni mpinzani mkubwa wa India katika michezo.

**Stephen Curry (US) - Mpira wa kikapu**

Nyota wa NBA Stephen Curry atacheza mechi yake ya kwanza ya Olimpiki mjini Paris.

Mlinzi wa timu ya Golden State Warriors, ni sehemu ya timu ya wanaume ya Marekani iliyo na nyota wengi ambao wanawinda medali ya 16 ya dhahabu ya Olimpiki. Wameshinda kila dhahabu tangu 2004.

Medali ya Olimpiki ndiyo kitu pekee kinachokosekana kwenye medali za Curry, ana mataji manne ya NBA, tuzo mbili za Mchezaji Bora wa NBA (MVP) na mbili za Kombe la Dunia.

LeBron James, mfungaji bora wa muda wote wa NBA, atacheza kwenye michezo hiyo kwa mara ya kwanza tangu London 2012, huku Kevin Durant akitafuta kuwa mwanariadha wa kwanza wa kiume kushinda medali nne za dhahabu za mpira wa kikapu.







Kona ya Urembo



# Urembo, utunzaji nywele kwa mwanamke

Na Unosye Atufigwege

NYWELE ni sehemu muhimu sana ya mwonekano wa mwanamke na zinaweza kumuathiri sana jinsi anavyojihisi na kuonekana.

Kwa wanawake wengi, nywele ni ishara ya urembo, afya, na hata utambulisho. Katika makala haya, tutazungumzia umuhimu wa nywele, aina mbalimbali za nywele, na mbinu bora za kuzitunza.

> Nywele zinahitaji unyevu ili ziweze kung'aa na kuwa na afya. Tumia mafuta ya nywele na bidhaa za unyevu zinazofaa aina ya nywele zako.

**Umuhimu wa nywele kwa mwanamke**

Kwa mwanamke, nywele zinaweza kuwa na maana kubwa zaidi ya urembo wa nje. Nywele zinaweza kuonyesha hali ya afya ya mtu, umri, na hata hali yake ya kihisia.

Nywele nzuri na zinazong'aa zinaweza kumfanya mwanamke ajihisi kujiamini na kuvutia zaidi. Kwa baadhi ya tamaduni, nywele zina maana za kidini na kitamaduni, ambapo zinaweza kuashiria hadhi ya kijamii au hali ya ndoa.

**Mbinu za kutunza nywele**

Kutunza nywele ni muhimu ili ziweze kuonekana nzuri na zenye afya. Zifuatazo ni baadhi ya mbinu bora za kutunza nywele:

**Kuosha na kuondoa uchafu**

Osha nywele zako mara kwa mara na tumia shampoo na 'conditioner' zinazofaa aina ya nywele zako. Epuka kuosha nywele kila siku ili kuepuka kuzifanya ziwe kavu.

**Unyevu**

Nywele zinahitaji unyevu ili ziweze kung'aa na kuwa na afya. Tumia mafuta ya nywele na bidhaa za unyevu zinazofaa aina ya nywele zako.

**Kupunguza matumizi ya joto**

Matumizi ya vifaa vya joto kama vile mashine za kusokota, kukausha, na kunyoosha nywele vinaweza kuharibu nywele. Tumia vifaa hivi kwa nadra na hakikisha unatumia dawa za kulinda nywele dhidi ya joto.

**Lishe bora**

Lishe yenye vitamini na madini muhimu kama vile vitamini E, A, na Omega-3 zinaweza kusaidia sana katika kuboresha afya ya nywele.

**Kukata ncha za nywele**

Kata ncha za nywele zako kila baada ya miezi mitatu ili kuondoa sehemu zilizoharibika na kuzuia nywele kugawanyika.

Kuna mambo kadhaa ambayo yanaweza kuharibu unadhifu na asili ya nywele kwa mwanamke kama haya hapa chini.

**Matumizi ya vyakula vya kichocheo**

Vyakula vyenye mafuta mengi, sukari na vichocheo vya kemikali vinaweza kuathiri afya ya nywele.

**Matumizi ya vitu vya kemikali**

Sabuni, dawa za nywele, na rangi zenye kemikali zinaweza kuharibu nywele na ngozi ya kichwa.



**Mchakato wa kujipamba**

Kutumia vifaa vya kupasha moto kama vile nyembe za moto, vipeperushi, na vifaa vya kunyolea nywele mara kwa mara kunaweza kufanya nywele kuwa kavu na dhaifu.

**Kutokuwepo kwa matunzo ya kila siku**

Kukosa kutunza nywele kwa kufuata taratibu za usafi, kutumia mafuta ya nywele, na kulala kwa taulo au mitandio iliyo safi kunaweza kuharibu nywele.

**Mabadiliko ya Hali ya Hewa**

Hali ya hewa kali, kama vile jua kali au mvua ya mara kwa mara, inaweza kuathiri nywele.

**Kumbuka;** Kujifunga nywele kwa nguvu au kutumia mikanda ya nywele yenye msuguano inaweza kuvunja nywele.

Kutunza nywele kwa kutumia bidhaa zinazofaa na kuzingatia lishe bora ni muhimu ili kuhakikisha unadhifu na afya bora ya nywele.

**Hitimisho**

Nywele ni sehemu muhimu sana ya urembo na utambulisho wa mwanamke. Kutunza nywele vizuri siyo tu kunaongeza mwonekano mzuri bali pia huongeza kujiamini na afya kwa ujumla.

Kwa kufuata mbinu za kutunza nywele na kuzingatia aina ya nywele zako, unaweza kuwa na nywele nzuri, zenye afya, na zinazovutia.






# Bola adai kuingizwa 'Mjini' na Singida BS

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Julai 31-Agosti 6, 2024 |

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA wa Singida Black Stars, Manu Bola ametishia kuiburuza timu hiyo Shirikisho la soka duniani (FIFA), akidai amevunjiwa mkataba pasipo kufuata taratibu huku na kutolipwa mishahara ya miezi mitatu ya Mei, Juni, Julai na bonasi kibao.

Bola anasema wakati anaondoka Lupopo na kujiunga na timu ya Ihefu (kwa sasa Singida) makubaliano yalikuwa kupelekwa Yanga baada ya msimu kumaliza, hivyo alisaini mkataba wa miaka miwili na nusu akitarajiwa kuitumikia Yanga kwa miaka miwili iliobaki huku Singida wakiendelea kumlipa kwa mujibu wa mkataba.

# Ahoua muuaji mpya Simba

## ● Rasmi kuwa kinara wa mashambulizi Msimbazi




**Na Mwandishi Wetu**

SIMBA imehitimisha maandalizi ya msimu mpya na sasa wanarejea Dar es Salaam kwa ajili ya Tamasha lao la utambulisho wa wachezaji na benchi la ufundi huku kiungo mshambulia mpya, Jean Charles Ahoua akitwaja ndiye mrithi wa mikoba ya Clatous Chama aliyehamia kwa mahasimu wao Yanga.

Kocha wao mpya, Fadlu Davids akizungumza baada ya wiki tatu za kujifua na kucheza mechi tatu za majaribio amewasifu wachezaji wake kwamba wengi wana vipaji asilia, lakini anahitaji muda kidogo wa kuitengeza safu yake ya ushambuliaji itakayoongozwa na Ahoua.

"Nina machaguo mengi ya wachezaji wazuri ambao umri wao pia ni mdogo na nguvu yao ndani ya uwanja itakuwa kubwa kwa sababu wana njaa ya mafanikio katika umri huo, hapo bado uwezo wa kukimbia kilometa nyingi upo na wananisikiliza ninachotaka," amedai Fadlu.

Ahoua(22) MVP wa Ligi Kuu ya Ivory Coast msimu uliopita, ndiye namba 10 mpya Simba kuelekea msimu mpya wa mashindano 2024-25, nafasi ambayo ilikuwa inachezwa na Chama kwa misimu kadhaa huko nyuma.

Mashabiki wa Simba na wadau wengi wa Soka nchini wanaona miguu ya Ahoua kama ndio itabeba sura ya muundo wa timu yao nzima kwa sababu ya ubora wake pamoja na sifa ambayo amekuja nayo kutoka Stella Club d'Adjamé ya nchini kwao

Kwenye mchezo wa kwanza wa kirafiki kule Ismailia Misri, alifunga mabao mawili dhidi ya Canal SC ambao walipoteza 3-0 mbele ya Simba!

Kuanzia usajili wake mpaka mchezo wa kirafiki aliofunga na hata kabla ya kufunga hayo mabao mawili amekuwa akitajwa sana kama miongoni mwa wachezaji bora ambao Simba SC imesajili katika dirisha hili.

Wengi wanamuona Ahoua kama sura ya timu kwenye muundo wa uchezaji wa Simba katika eneo la ubunifu ambalo linahitaji mtu mwenye ubora wa hali ya juu!

Mbali ya Ahoua ambaye ni bora kwenye utengenezaji wa nafasi, lakini pia Simba inahitaji miguu bora na yenye ufanisi wa juu kutoka kwa wachezaji wengine kama Willy Onana, Joshua Mutale, Steve Mukwala, Freddy Koublan, na wengineo hasa viungo ambao atacheza karibu nao wakina, Deborah Fernandes Mavambo, Fabrice Ngoma, Muzamili Yassin, Awesu Ally Awesu, na Omari

# GSM yaongeza udhamini Yanga

**Na Mwandishi Wetu**




CEO wa Kampuni ya GSM, Benson Mahenya ametangaza rasmi kuwa, kupitia kampuni yao mpya ya vinywaji, wameingia mkataba wa miaka mitano na klabu ya Yanga wenye thamani ya shilingi bilioni 1.

"Kwa niaba ya GSM Group tunayo furaha ya kutangaza rasmi kuwa tumepanua wigo wa mahusiano yetu na klabu ya Yanga SC, tunatangaza rasmi kuwa kampuni mpya ya vinywaji, imeingia mkataba wa miaka mitano na klabu hii, amesema Mahenya CEO wa GSM Group

Naye Mkurugenzi wa Sheria wa Yanga, Patrick Simon amepasha kuwa, mbali ya udhamini huo wa vinywaji kupitia Kampuni ya GSM Beverage, pia wameongeza mkataba mwingine na Benki ya Equity.

"Leo tumekuja hapa kuwatangazia wadhamini wetu kuelekea kilele cha wiki ya Mwananchi, mdhamini mkuu wa wiki ya mwananchi ni Benki ya CRDB, hata hivyo tumeongeza washirika wengine Benki ya Equity pamoja na GSM Beverage," amenena Simoni Patrick.

Naye Msemaji wa Yanga, Haji Manara ametamba kuwa, watawafunga Watani wao wa jadi Simba si chini ya bao 4-0 kwenye pambano lao nusu fainali ya Ngao ya Jamii Agosti 8.

Siyo mechi hiyo ya Ngao ya Jamii tu, Haji ametamba kuwa, hata kwenye Ligi Kuu ya Vodacom hakuna timu ya kuwazuia kuendelea kutetea taji lao na watafanya hivyo hadi mwaka 2030.